# Nipashe

Jumatano Aprili 14, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580550

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Waliopisha** bomba la mafuta kulipwa Julai

UKURASA 3



**Serikali** kununua mitungi ya gesi kupambana na corona

UKURASA 4




**United wamtaka tena Sancho**

UKURASA 20

# Serikali yawaahidi neema watumishi

• **Ni** nyonge-za mishahara, kupandishwa mada-raja. Yamo maslahi kwa wastaafu...

*Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohammed Mchengelwa

## Rais Mwinyi awatumbua makamanda madai ufisadi

UKURASA 2

## Wadau kushirikishwa kanuni mpya kikokotoo cha mafao

UKURASA 3


**MICHEZO** MWAMBUSI AGAWA DOZI GONJWA YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Serikali yawaahidi neema watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amesema atazingatia maslahi ya watumishi wa umma ikiwamo nyongeza ya mishahara, malipo ya wastaafu na kupandiswa kwa madaraja kwa mujibu wa sheria.

Mchengerwa alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na watumishi wa wizara hiyo katika kikao kazi pamoja na kujitambulisha rasmi.

Alisema akiwa katika nafasi hiyo, moja ya vipaumbele vyake itakuwa kuhakikisha maslahi ya watumishi wa umma yanazingatiwa ili kuongoza ufanisi na kuleta tija katika maeneo mbalimbali.

Masuala kama nyongeza ya mishara, kupandishwa kwa madaraja ya watumishi, malipo ya wastafu, alsiema ni mambo ambayo yapo kwa mujibu wa sheria hivyo utekelezaji wake ni wa lazima na si hiari.

"Mtumishi kuongezwa mshahara, kupandishwa madara au kupandishwa vyeo haya yapo kwa mujibu wa sheria na si ombi wala huruma ya mwajiri wake, hivyo tutahakikisha tunatekeleza kwa mujibu wa sheria inavyoelekeza," alisema Mchengerwa

Pia alsiema alisema pamekuwapo na malalamiko ya watumishi wa umma juu ya kupandishwa madaraja kazini na wengi wao kukaimu nafasi kwa muda mrefu.

"Sheria inatutaka kupadisha madaraja mtumishi kwa muda fulani lakini wengi bado hawajapatiwa haki yao, hivyo tutahakikisha tunafanya kwa kuzingatia sheria," alisema.

Waziri pia alipiga marufuku watumishi kukaimishwa nafasi moja kwa zaidi ya miezi sita kama ambavyo imekuwa mazoea katika utumishi wa umma katika maeneo mbalimbali.

"Sheria inakataza mtumishi kukaimishwa katika nafasi kwa miezi sita lakini leo hii kuna maeneo wako watu wamekaimu kwa zaidi ya miaka sita, hivyo kuanzia leo (juzi) ni marufuku mtu kukaimu zaidi ya miezi sita" alisisitiza Mchengerwa.

Pia alisema moja ya maeneo ambayo watayafanyia kazi pia ni pamoja na malalamiko ya malipo ya wastaafu kucheleweshwa na kuwapa wakati mgumu kumudu maisha yao na familia zao.

Alisema watumishi wengi ambao wamemaliza muda wao wa kulitumikia taifa na kustaafu kwa mujibu wa sheria, bado wamekuwa wakikumbana na kero ya kucheleweshewa malipo kinyume cha sheria.

"Haki hizi kwa mtumishi aliyefanya kazi kwa kuzingatia kanuni na maadili ya utumishi wa umma ni jambo la lazima na si la kuomba, hivyo ni lazima azipate kama sheria inavyoelekeza" alisema Mchengerwa

Kadhalika alisema kuwa katika uongozi wake atahakikisha stahiki zote za mtumishi zinapatiknaa kwa wakati ili kuongeza morali kwa kujituma katika maeneo yao.

Vilevile, aliwataka wakuu wa wilaya wa mikoa ambao wamekuwa na tibia ya kutumia mamlaka yao vibaya kwa kuwaweka ndani watumishi, kuacha mara moja na kutumia busara.

"Serikali inazingatia sheria na utawala bora. Niwaombe viongozi wenzangu kutumia busara pale inapobidi kwani kumekuwapo na viongozi wanafanya mambo ambayo yanakiuka hata katiba ya nchi. Viongozi wote wanatakiwa kufanya mambo kwa kuzingatia kanuni na sheria," alisema Mchengerwa.



Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania, wakiuombea mwili wa aliyekua Askofu wa Kanisa Katoliki Njombe, Hayati Alfred Maluma, kabla ya mazishi yake yaliyofanyika ndani ya kanisa hilo, jana. Habari ukurasa wa 4. **PICHA: ELIZA KILINDI.**

# Rais Mwinyi atengua makamanda 3

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametengua uteuzi wa makamanda watatu wa Idara Maalum za SMZ baada ya kubainika wafanyakazi hewa na kusababisha upotevu wa mabilioni ya fedha za serikali.

Waliotenguliwa ni Kamanda wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar Ali Abdallah Ali, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kanali Ali Mtumweni Hamad na Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Comodore Hassan Mussa Mzee.

Akitoa taarifa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari, Ikulu Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema kufuatia taarifa za uwapo wa wafanyakazi hewa katika Idara Maalum za SMZ, aliunda kamati ya uchunguzi kwa kufanya uhakiki wa idadi ya wafanyakazi pamoja na viwango vya mishahara vinavyotolewa kwa vikosi vyote.

Alisema ripoti ya Kamati ya Uhakiki iliyomfikia ilieleza kulikuwa na wafanyakazi 381 waliokuwa wakilipwa mishahara bila ya kuwa katika utaratibu (watumishi hewa).

Alisema fedha zilikuwa zikipokelewa na kutumika katika kipindi chote na walikuwa katika vikosi hivyo, na kueleza kuwa lililothibitika ni wakati Kamati imeanza kazi zake baadhi ya vikosi kikiwamo JKU kuanza kutengeneza utaratibu wa kurasimisha uwapo wa wafanyakazi hao hewa.

Alisema waliwahi kukamatwa baadhi ya maofisa katika nyumba ya mtu binafsi wakiwa wamewavalisha sare za jeshi na kuwapiga picha ili kuthibitisha wamo katika ajira rasmi.

Rais Dk. Mwinyi alisema imebainika kuwa fedha zilizotumika kwa upotevu ni Sh. 2,235,725,000.00 kutokana na fedha zilizokuwa zikitumika kwa wafanyakazi hewa.

Vile vile, Rais Dk. Mwinyi alisema Kamati ilikwenda kuhakiki ulipaji wa posho katika vikosi hivyo na kubaini wastani wa upotevu wa fedha zilizokuwa zikilipwa kwa ajili ya posho kwa mwezi wa Desemba ni jumla ya Sh. 304,135,939.00 sawa na wastani wa Sh. 1,824,815,634.00 kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba.

Alisema Kamati haikuishia hapo na iliendelea kubaini kuna watumishi ambao walikuwa wameshastaafu, lakini bado walikuwa wakiendelea kupokea mishahara na kuliwa na wastaafu 12 wa Idara Maalum za SMZ waliokuwa wakiendelea kulipwa mishahara baada ya kustaafu kinyume na utaratibu.

Alisema hali hiyo imesababishwa na uzembe wa wahasibu wakuu wa Idara Maalum za SMZ ama kwa kukusudia na kwa misingi hiyo serikali imeingia hasara ya jumla ya Sh. milioni 44,610,280.00.

Hata hivyo, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa wastaafu wawili waliitwa na Kamati na kuhojiwa na baadae walikubali kurejesha fedha jumla ya Sh. milioni 10,766,560.00 fedha ambazo ziliingizwa katika mfuko mkuu wa serikali.

Rais Dk. Mwinyi alisema mtumishi anapofukuzwa kazi hutakiwa kuwekewa kizuizi cha mishahara mara tu anapofukuzwa kazi hata hivyo, Kamati imegundua kwamba wahasibu wakuu wa vikosi pamoja na waingizaji wa taarifa za mishahara huchelewesha mchakato huo kwa makusudi ili fedha hizo zitumike katika matumizi yao binafsi.

Kamati imegundua wahasibu huwatengenezea madeni watumishi waliokuwa wamefukuzwa kazi na fedha hizo hukatwa na kupelekwa kwenye duka la kikosi na hatimaye fedha hizo huingia mifukoni mwa wahasibu hao na jumla ya fedha zilizopotea kwa aina hiyo ni kiasi cha Sh. 117,724,000.00.

Aidha, alisema kuwa Kamati imebaini kuna ukataji wa posho ya chakula kwa askari Kapera kinyume na utaratibu kwa kuwa kwa kawaida askari anapoajiriwa hukaa kambini kwa kipindi cha miaka miwili na kukatwa posho ya chakula Sh. 70,000 kila askari kwa mwezi, fedha ya kujikimu.

Alisema kwa upande wa JKU Kamati imebaini jumla ya askari 771 walikatwa fedha za posho ya chakula bila kukaa kambini na fedha zao kuingia mifukoni mwa watu wachache kiasi cha Sh. 539,700,000.00 kwa kipindi cha miezi 10 kuanzia mwezi wa Machi 2020 hadi Desemba 2020.

Pia, Kamati hiyo imebaini maofisa na askari wananyimwa fursa ya kupata vielelezo vya taarifa za mishahara yao ikiwamo 'Pay slip' zao na kusababisha baadhi ya askari hao kukatwa mishahara yao kinyume na utaratibu na kutokujua malengo ya makato hayo.

Alisema kuwa Kamati hiyo pia, imegundua kuna baadhi ya askari waliokuwa wakiingiziwa posho na kukatwa kwa kuingizwa kwenye maduka ya vikosi hali ambayo iliibua malalamiko mengi kwa askari na kuwakosesha morali ya kufanya kazi.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa takriban askari wote walikiri kuwa kwa mara ya kwanza baada ya kuanza uhakiki huo ndipo wamepewa 'Pay slip' zao pamoja na kujua stahiki zao.

Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa pamoja na Kamati kufanya kazi nyingi na kugundua udhaifu sehemu nyingi, inatosha kwa hayo yaliobainika kuchukua hatua za kisheria na kuagiza wahasibu na waingizaji wa data wachukuliwe hatua za kisheria na tayari wameshasimamishwa kazi na utaratibu wa kuchukuliwa hatua za kisheria unaendelea.

## HABARI KITAIFA

# Ndalichako: Maadili ya uongozi tatizo

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema taifa linakabiliwa na changamoto zinazohusu nidhamu na maadili ya kiuongozi katika nyanja mbalimbali za kiutendaji huku viongozi wakikwepa kuwajibika.

Prof. Ndalichako aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya kumbukizi ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, yaliyoandaliwa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kigamboni.

Maadhimisho hayo yalibebwa na kauli mbiu isemayo, "Falsafa ya Mwalimu Nyerere katika elimu na uchumi kwa ajili ya maendeleo ya jamii."

Prof. Ndalichako ambaye alikwenda hapo kumuwakilisha Makamu wa Rais, Dk.Philip Mpango, alisema tatizo la nidhamu katika utumishi na uwajibikaji bado ni kubwa.

"Ninafurahi chuo kinatoa mafunzo kuhakikisha wanawajenga watu wenye sifa za uongozi, maadili na wanaotambua misingi ya taifa ya kudumisha amani, umoja na mshikamano," Prof. Ndalichako alisema.

Alisema kwa sasa wanawaweza kukuta katika taasisi jambo linatokea ambalo linahitaji uongozi kukaa pamoja na kufanya uamuzi.

"Lakini jambo hilo lililofanyiwa uamuzi lisipokuwa na matokeo mazuri kwenye jamii baadhi ya viongozi walioshiriki katika uamuzi wanadhubutu kusema ni jambo la ovyo wakati na wao walikuwa sehemu ya uamuzi," alisema.

"Ni maoni ya Watanzania na wadau wa elimu kwamba hawajapikwa vizuri, hawajaiva sawasawa, hawaendani na matarajio ya soko la ajira na waajiri, nimuhimu tufanye tathmini kujiridhisha kwamba elimu inakidhi na pale kwenye upungufu tuchukue hatua stahiki," alisema.

Prof. Ndalichako alitumia jukwaa hilo kumuahidi Rais Samia Suluhu Hassan kuwa hata muangusha, atafanya kazi kwa bidii na weledi na kuhakikisha anatumia maarifa yake ili malengo ya serikali katika sekta hiyo yanatimia.

Mkuu wa Chuo hicho. Prof. Shadrack Mwakalila, alisema kwa kutambua umuhimu wa uongozi na maadili chuo kimeliweka somo hilo katika ngazi mbalimbali za masomo ili wanafunzi waweze kunufaika nalo.

Mwenyekiti wa Bodi ya chuo hicho, Stephen Wasira, alieleza historia ya Mwalimu Nyerere tangu shule ya msingi hadi aliposhika wadhifa mkubwa wa nchi na mchango mkubwa alioutoa kwa ukombozi Kusini mwa Afrika.

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mstaafu, Ludovic Otouh, katika mada yake ya sekta ya elimu kwa maendeleo ya jamii, alitaka serikali iingilie kati suala la mafunzo kwa vitendo maofisini ili yatolewe kuwawezesha wanafunzi kuongeza ujuzi.

# Serikali yafunguka kikokotoo mafao wastaafu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

UKIWA umebaki mwaka mmoja kabla ya kuanza kutumika kwa kikokotoo kipya katika ulipaji wa mafao ya wastaafu, serikali imesema itashirikiana na wadau kupata kanuni za ulipaji wa mafao hayo zitakazokidhi matarajio ya wafanyakazi.

Oktoba 20, 2017, Bunge lilipitisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambayo mbali na kuunganisha mifuko ya pensheni kuunda Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSF) na kufanya marekebisho kwenye Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kanuni zake ziliweka utaratibu wa kulipa mafao kwa mkupuo kwa asilimia 25 na asilimia 75 inayobaki kulipwa kama mshahara kwa mstaafu kwa miaka 12.5.

Sheria hiyo ambayo pia iliweka umri wa kustaafu kuwa miaka 55 kwa hiyari na miaka 60 kwa lazima (kwa kada maalum kama vile madaktari na maprofesa umri wa kustaafu ni miaka 60 kwa hiari na miaka 65 kwa lazima), iliibua mjadala mkali kitaifa uliosababisha aliyekuwa Rais kipindi hicho, Hayati Dk. John Magufuli, kuingilia kati akiagiza kikokotoo hicho kipya kianze kutumika mwaka 2023.

Akiwasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema serikali itashirikisha wadau katika uandaaji wa kanuni za ulipaji mafao.

"Katika mwaka 2021/22, serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ili kuwezesha kupata kanuni za ulipaji wa mafao ambazo zinakidhi matarajio ya wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi," alisema.

Aprili 6 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliweka wazi kuwa PSSF iko katika hali mbaya kifedha, akisema: "Najua hali ya PSSF, kuwa mfuko huu una halai mbaya na ndiyo maana sikuteua mtu. Hapa tuna kazi ya kufanya kwanza kunusuru mfuko ule halafu ndiyo tujue sasa safu ipi ya kushika huo mfuko."

Mfuko huo ni zao la kuunganishwa kwa mifuko minne ambayo ni: PPF, PSPF, LAPF na GEPF.

Katika hotuba yake ya jana, Majaliwa pia alisema serikali itaendelea kuisimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha Sera ya Kinga ya Jamii inakamilika.

Alisema ofisi yake itaendelea kutekeleza majukumu yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Hifadhi ya Jamii, ili kuhakikisha taasisi zote za Hifadhi ya Jamii zinafuata kanuni na miongozo iliyopo ili kupunguza kero kwa wananchi wanaowahudumia.

Majaliwa alibainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha, gharama za uendeshaji wa mifuko zimeendelea kupungua kutoka asilimia 6.8 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 5.4 Desemba 2020.

Alibainisha kuwa sambamba na kushuka kwa gharama za uendeshaji, mifuko ya pensheni imeendelea kulipa mafao kwa wastaafu.

"Hadi kufikia Machi mwaka huu, jumla ya wanachama 203,418 walilipwa mafao ya pensheni ya Sh. trilioni 1.361," Majaliwa alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi (kulia), akinunua mahitaji mbalimbali kwa ajili ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, katika soko la mashine tatu, mjini Iringa, wakati wa ziara yake ya kukagua masoko, juzi. **PICHA NA FRANCIS GODWIN**.

# Wananchi waliopisha bomba la mafuta kulipwa fidia Julai

**Na Elizabeth Zaya**

WANANCHI wanaotakiwa kupisha mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, nchini Uganda hadi Tanga, wanatarajiwa kuanza kulipwa fidia zao Julai, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, jijini Dar es Salaam kuelezea maeneo mbalimbali ambayo Watanzania watanufaika kutokana na mradi huo, Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), James Mataragio, alisema zaidi ya Sh. bilioni 20 zinatarajiwa kulipwa kwa waathirika walioopitiwa na mradi huo.

"Kama mnavyofahamu tathmini kwa waathirika ilishafanyika tangu mwaka 2019 na kwa sababu mradi unaanza, hivyo kufikia Julai, mwaka huu tutakuwa tumeanza kulipa wote waathirika na hakuna athari za mazingira kwa sababu bomba limepita katika sehemu ambazo hazina athari kubwa sana," alisema Mataragio.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nishati, Dk. Medadi Kalemani, utekelezaji wa mradi huo unatarajia kuanza mwezi huu na utapitia katika mikoa nane, wilaya 24, vijiji 127, na vitongoji 502.

Mataragio alitaja baadhi ya maeneo ambayo Watanzania watanufaika kupitia mradi huo kuwa ni ajira, eneo la ununuzi wa vifaa vitakavyohitajika wakati wa ujenzi wa mradi na kwamba kazi ambazo zimetengwa kwa ajili ya ushiriki wa Watanzania pekee ni pamoja na eneo la usafirishaji wa mabomba na vifaa vingine vitakavyotumika kwenye mradi.

absa

Hongera kwa uteuzi
Dkt. Philip Isdor Mpango

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wote wa Benki ya Absa tunapenda kumpongeza Mh. Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamtakia kila la kheri katika uongozi wake.



Absa Bank Tanzania Limited (yenye usajili namba 38557) inaongozwa na kanuni za Benki Kuu ya Tanzania.

# Maelfu wamzika Askofu Maluma

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAMIA ya wananchi jana walijitokeza katika ibada ya mazishi ya aliyekuwa Askofu wa Katoliki Njombe, Alfred Maluma, baadaye kuzikwa katika makaburi maalumu yaliyopo ndani ya Kanisa Katoliki la Njombe.

Askofu Maluma alifariki Aprili 6, mwaka huu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa akipatiwa matibabu.

Akitoa salamu za rambirambi katika mazishi hayo kwa niaba ya Waziri Mkuu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliwataka Watanzania kuiombea nchi, kudumisha amani, upendo na mshikamano.

Alisema Askofu Maluma enzi za uhai wake alijitolea kufanya kazi ya kiroho na kusaidia maendeleo ya kanisa na wananchi wa Njombe kwa ujumla.

Awali akimkaribisha Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, alisema Askofu Maluma alikuwa kiongozi mpole, mnyenyekevu na mwenye kujitolea.

Naye, Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, alitoa pole kwa mapadri, watawa na waamini wa Jimbo la Njombe na wananchi kwa ujumla kwa kifo cha Askofu Maluma.

Alisema sifa zake zilizotajwa na ambazo hazikutajwa ni za kweli, hivyo unapoondokewa na mtu mwenye sifa hizo wengi huumia moyoni.

Askofu Nyaisonga alisema: "Tupokee msiba huu kwa imani na utulivu, tunatoa neno la shukrani kwa wote waliomhangaikia alipokuwa anatibiwa mkoani Morogoro na Dar es Salaam".

# Serikali kugawa mitungi Oksijeni kukabili corona

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imeagiza mitambo saba yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 ya hewa ya Oksijeni kwa siku ikiwa ni sehemu ya mikakati yake katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, ikiwamo homa kali ya mapafu.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alibainisha kuwapo kwa mkakati huo alipowasilisha bungeni jana hotuba ya mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuwa mitambo hiyo iliagizwa Februari, mwaka huu na itasimikwa kwenye hospitali za rufani za mikoa za Amana, Dodoma, Geita, Manyara, Mbeya, Mtwara na Ruvuma.

"Sambamba na usimikaji wa mitambo hiyo, hospitali zote saba zimepatiwa mitungi 74 kila moja. Kila mtambo kwenye hospitali hizo utakuwa na uwezo wa kusambaza gesi ya Oksijeni katika vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 18.

"Hatua hiyo, inalenga kuimarisha mfumo wa huduma za afya ili kuwa tayari kukabiliana na changamoto za sasa na baadaye. Maeneo yanayolengwa ni vyumba vya kutoa huduma za dharura, huduma ya mama na mtoto, upasuaji na vyumba vya uangalizi maalum," alisema.

Majaliwa alibainisha kuwa katika mwaka ujao wa fedha, serikali itaongeza mitambo mingine ya aina hiyo 12.

Vilevile, Waziri Mkuu aligusia maendeleo ya ujenzi wa hospitali tatu za rufani za kanda ambazo ni Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini - Mtwara (umefikia asilimia 90), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya (asilimia 72) na Kanda ya Ziwa - Burigi (awamu ya kwanza asilimia 98).

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya uchunguzi kwa njia ya maabara katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto - Kilimanjaro, ujenzi na ukarabati wa hospitali za halmashauri 102, vituo vya afya 487 na ujenzi wa zahanati 1,198.

Kuhusu Sekta ya Nishati, Majaliwa alisema utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Mw 2115 umefikia asilimia 45 hadi Machi mwaka huu, zikitumika Sh. trilioni 2.1 huku zikizalishwa ajira 7,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Mradi huo una thamani ya Sh. trilioni 6.55.

Kuhusu masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, Majaliwa alisema soko la minofu ya samaki aina ya sangara limepatikana Saudi Arabia na soko la nyama katika nchi za Kuwait, Qatar na Oman.

Waziri Mkuu pia alisema soko la matunda aina ya karakara (passion), parachichi na nanasi limepatikana katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Alibainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha, zaidi ya tani 7,000 za nyama na kontena 22 za matunda ziliuzwa katika masoko hayo.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha, Majaliwa aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 116.784. Kati yake, Sh. bilioni 93.303 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 23.481 za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Majaliwa pia aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 128.873 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 121.876 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 6.997 ni kwa ajili ya maendeleo.

# Majaliwa: Ndege mpya tatu zinakuja



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisoma hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI kukiwa na kilio cha wadau kuhusu Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kutengeneza hasara ya mabilioni ya shilingi, serikali imesema imekamilisha malipo ya ndege mpya tatu.

Akiwasilisha bungeni jana makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka 2021/22, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliiarifu Bunge kuwa ndege hizo zinatarajiwa kuwasili nchini katika mwaka ujao wa fedha.

Majaliwa alisema kuwa sambamba na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa anga, serikali imekamilisha malipo ya ununuzi wa ndege mpya tatu.

Alibainisha kuwa kati ya ndege hizo, mbili ni aina ya Airbus A220-300 na nyingine ni Dash 8-Q400 De-Havilland, na kuiwezesha serikali kuwa na ndege 12.

"Nitumie fursa hii kulipongeza Shirika la Ndege Tanzania kwa kuanzisha safari za kwenda Guangzhou, China. Safari hizo zitakuwa chachu ya kuimarisha biashara, utalii na ajira," alisema.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20 imeibua mjadala mkali kuhusu hatua hiyo ya serikali kununua ndege mpya, baada ya kubainisha kuwa ATCL imetengeneza hasara ya mabilioni kwa miaka mitano mfululizo.

Katika ripoti yake hiyo iliyowasilishwa bungeni Alhamisi ya wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa hadi kufikia Juni 30, mwaka jana, serikali ilikuwa imenunua ndege nane kwa gharama ya Sh. trilioni 1.028 katika juhudi ya kuifufua ATCL.

"Ndege hizo zinamilikiwa na Wakala wa Ndege za Serikali na ATCL huzikodisha. Pamoja na kununua ndege, kwa miaka mitano, yaani kuanzia 2015/16 hadi 2019/20, serikali imeisaidia ATCL kiasi cha Sh. bilioni 153.711 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na maendeleo.

"ATCL imekuwa ikitengeneza hasara kwa miaka mitano mfululizo na mwaka huu (2019/20) ilitengeneza hasara ya Sh. bilioni 60.246. Kwa miaka mitano, imetengeneza hasara ya Sh. bilioni 153.542," CAG anabainisha kwenye ripoti yake hiyo.

Akifafanua zaidi kuhusu Sekta ya Uchukuzi, Majaliwa alisema serikali pia imekamilisha utaratibu wa ununuzi wa vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo na abiria, huku akifafanua kuwa kuboreshwa kwa miundombinu ya reli ili kutarahisisha usafirishaji wa mizigo ya ndani na nchi jirani.

## TANGAZO

# TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA - NMB BANK PLC

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

**NMB** Karibu yako

**Trilioni 4.1** Mikopo Halisi Iliyopo **14%** YoY

**Trilioni 7.1** Jumla ya Mali **8%** YoY

**Trilioni 5.2** Amana za Wateja **7%** YoY

**Faida** kabla ya Kodi ya Mapato **Bilioni 295.7** **40%** YoY

**Faida** Baada ya Kodi ya Mapato **Bilioni 205.8** **45%** YoY

Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa **18%**

Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi **5%**

Uwiano wa Matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi **51%**

*YoY - Linganishi mwaka kwa mwaka

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Mwaka uliyopita 31.12.19 | Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Mwaka uliyopita 31.12.19 |
| **A.** | **MALI** | | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 661,689 | 498,231 | 661,689 | 498,231 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 385,799 | 842,909 | 385,799 | 842,909 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,304,253 | 761,554 | 1,304,253 | 761,554 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 170,829 | 264,326 | 170,829 | 264,326 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 1,449 | 4,152 | 1,449 | 4,152 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 4,108,789 | 3,590,006 | 4,109,260 | 3,595,688 |
| 12 | Mali Nyingine | 206,893 | 214,162 | 280,336 | 383,191 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 2,920 | 2,920 | 2,920 | 2,920 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 215,715 | 239,167 | 181,562 | 203,044 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **7,058,336** | **6,417,427** | **7,098,097** | **6,556,015** |
| **B.** | **DHIMA** | | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 131,224 | 33,446 | 131,224 | 33,446 |
| 18 | Amana za Wateja | 5,247,973 | 4,882,123 | 5,247,978 | 4,887,850 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 36,645 | 19,833 | 36,645 | 19,833 |
| 20 | Amana Maalumu | 40,833 | 14,595 | 40,833 | 14,595 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,118 | - | 2,118 | 2,133 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 36,682 | 33,355 | 36,683 | 33,355 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadaye | - | - | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 107,977 | 117,530 | 148,943 | 244,971 |
| 28 | Madeni | 323,740 | 347,443 | 323,740 | 347,443 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **5,927,191** | **5,448,325** | **5,968,163** | **5,583,626** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **1,131,145** | **969,102** | **1,129,934** | **972,389** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 896,141 | 799,733 | 903,340 | 809,173 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 210,300 | 144,739 | 205,802 | 142,167 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 792 | 1,049 | 792 | 1,049 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 3,912 | 3,581 | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **1,131,145** | **969,102** | **1,129,934** | **972,389** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 624,881 | 652,654 | 624,881 | 652,654 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 231,287 | 254,241 | 231,287 | 254,241 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 204,809 | 173,110 | 204,809 | 173,110 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 10,055 | 2,850 | 10,055 | 2,850 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 15% | 16% | 15% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5% | 7% | 5% | 7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 78% | 73% | 78% | 73% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58% | 56% | 58% | 55% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79% | 72% | 79% | 71% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 8% | 14% | 8% | 14% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 10% | 13% | 8% | 15% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 712,648 | 653,195 | 712,977 | 653,974 |
| 2 | Gharama za Riba | (141,483) | (130,820) | (147,322) | (136,333) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **571,165** | **522,375** | **565,655** | **517,641** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (119,312) | (100,410) | (119,312) | (100,410) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **271,279** | **204,409** | **271,279** | **204,409** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 30,484 | 25,554 | 30,484 | 25,554 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 226,400 | 169,153 | 226,400 | 169,153 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 14,395 | 9,702 | 14,395 | 9,702 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(421,852)** | **(410,513)** | **(421,879)** | **(410,552)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (195,515) | (182,579) | (195,515) | (182,579) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (10,603) | (10,793) | (10,603) | (10,793) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (215,734) | (217,141) | (215,761) | (217,180) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **301,280** | **215,861** | **295,743** | **211,088** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (90,980) | (71,122) | (89,941) | (68,921) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **210,300** | **144,739** | **205,802** | **142,167** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **(257)** | **168** | **(257)** | **168** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **210,043** | **144,907** | **205,545** | **142,335** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,474 | 3,450 | 3,474 | 3,450 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 420 | 289 | 412 | 284 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 420 | 289 | 412 | 284 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Mali | 3% | 2% | 3% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 19% | 15% | 18% | 15% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 50% | 56% | 51% | 57% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 10% | 11% | 13% | 14% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | KUNDI | | BENKI | |
|---|---|---|---|---|
| | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31.12.2020 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31.12.2019 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 301,280 | 215,861 | 295,743 | 211,088 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 68,308 | 73,367 | 68,550 | 73,608 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (518,783) | (348,605) | (513,572) | (343,894) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (159) | (131) | (159) | (131) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 506,677 | 614,007 | 500,955 | 607,347 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (7,970) | (2,717) | (12,202) | (2,717) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 42,333 | 36,843 | 49,370 | 54,422 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 28,297 | (18,499) | 30,247 | (33,659) |
| - Kodi Iliyolipwa | (123,140) | (60,418) | (122,089) | (56,357) |
| - Mengineyo (bainisha) | 64,078 | 10,003 | 64,078 | 10,003 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **360,921** | **519,710** | **360,921** | **519,710** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (18,755) | (12,649) | (18,755) | (12,649) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 174 | 292 | 174 | 292 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (1,096,690) | (659,892) | (1,096,690) | (659,892) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 560,401 | 641,480 | 560,401 | 641,480 |
| Mengineyo (Matokeo ya mabadiliko katika fedha za kigeni) | (4,325) | (10,967) | (4,325) | (10,967) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(559,195)** | **(41,736)** | **(559,195)** | **(41,736)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (48,000) | (33,000) | (48,000) | (33,000) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (67,297) | (71,102) | (67,297) | (71,102) |
| Mengineyo (bainisha) | (11,944) | (60) | (11,944) | (60) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(127,241)** | **(104,162)** | **(127,241)** | **(104,162)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(325,515)** | **373,812** | **(325,515)** | **373,812** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 1,232,544 | 858,732 | 1,232,544 | 858,732 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **907,029** | **1,232,544** | **907,029** | **1,232,544** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **951,340** | - | - | **1,049** | **972,389** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 205,802 | - | - | - | 205,802 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (257) | (257) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,109,142** | - | - | **792** | **1,129,934** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **808,448** | - | **33,725** | **881** | **863,054** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 142,167 | - | - | - | 142,167 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **951,340** | - | - | **1,049** | **972,389** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **944,472** | - | - | **4,630** | **969,102** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 209,969 | - | - | 331 | 210,300 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (257) | (257) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **1,106,441** | - | - | **4,704** | **1,131,145** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | - | **799,128** | - | **33,725** | **4,342** | **857,195** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 144,619 | - | - | 120 | 144,739 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 33,725 | - | (33,725) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | 168 | 168 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | - | **944,472** | - | - | **4,630** | **969,102** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAOISHIA DESEMBA 2020

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Afisa Mtendaji Mkuu** | [signature] | Machi 30, 2021 |
| Juma Kimori<br>**Afisa Mkuu wa Fedha** | [signature] | Machi 30, 2021 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | [signature] | Machi 30, 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na PricewaterhouseCoopers, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | [signature] | Machi 30, 2021 |
| Leonard Mususa<br>**Mkurugenzi** | [signature] | Machi 30, 2021 |

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha wafanyakazi kipate jawabu Mei Mosi

**JUZI** Rais wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (TUCTA), alieleza matarajio makubwa waliyonayo kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kuelekea maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Mei Mosi.

Matarajio ambayo yamekuwa kilio cha muda mrefu ni nyongeza ya mishahara ambayo haijafanyika kwa miaka mitano, huku bei za bidhaa na vyakula zikipanda na kushuka kila wakati, jambo ambalo limechangia kupungua kwa morali ya kazi.

Kwa miaka mitano serikali haijaongeza mishahara ya wafanyakazi na ahadi kubwa ilikuwa ni kufanya hivyo.

Februari 8,2019, Waziri Mkuu akijibu swali la aliyekuwa Mbunge wa Mbozi, Pascal Haonga, juu ya ongezeko la mishahara kwa watumishi, aliwataka kuwa na subira wakati serikali inaendelea na mchakato wa kuwatambua watumishi wa umma halali na kufanya ulinganifu katika kada mbalimbali, ili waanze kulipwa mishahara stahiki.

Wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2020, aliyekuwa mgombea urais wa CCM, ambacho ndiyo kimeunda serikali, katika moja ya ahadi zake ni ongezeko la mishahara kwa watumishi.

Februari 11, mwaka huu, akijibu swali la Mbunge wa Konde, Khatibu Said Haji, katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, aliwataka watumishi wasikate tamaa kwa vile mishahara mipya haijatangazwa na badala yake wachape kazi kwa kuwa maslahi yao yanaendelea kuboreshwa.

Kwamba serikali ya awamu ya tano ilivyoingia madarakani ilibaini kwamba ikitangaza kupandisha mishahara, itaumiza watu wengi kwa kuwa gharama za bidhaa hupandishwa haraka. Pia, inapotangaza mishahara kupanda inapelekea ugumu wa maisha kwa kuwa huduma nyingine kwenye masoko ama usafiri wa mabasi zinapanda.

Lakini pia, kupandisha mshahara kwa Sh. 20,000 au 30,000 hakuna tija kwa watumishi bali kupunguza kodi kunamsaidia zaidi mfanyakazi.

Kwa sasa kodi ya mshahara (PAYE) ni imeanzia digiti moja yaani asilimia 9 kutoka digiti mbili za awali, huku ikitofautiana kwa kiwango cha mishahara jambo ambalo limetoa ahueni kubwa kwa wafanyakazi, huku kilio cha nyongeza ya mishahara kikiwa pale pale.

Mfumuko wa bei umedhibitiwa kwa kiasi kikubwa, lakini gharama za maisha zimepanda hasa kwenye makazi na huduma nyinginezo ambazo mfanyakazi atahitaji kugharamia.

Mara nyingi utaratibu wa kupandisha mishahara uko zaidi serikalini, huku sekta binafsi, ikiwa ni kwa mujibu wa taratibu za kampuni husika, ambazo mara nyingi hutegemea na hali ya uchumi na ukuaji wa mzunguko wa fedha pamoja na ushindani.

Kilio cha Rais wa TUCTA ni cha watumishi wote wa umma ambao kwa muda mrefu wamesubiri kusikia nyongeza ambayo italeta mabadiliko kwa mtu mmoja mmoja kwa sasa na hata baada ya kumaliza muda wa utumishi wake.


Ni muhimu serikali ikatilia maanani kilio hiki na kufikiria uwezekano wa kuongeza mshahara, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yao kwa watumishi.

Hali hiyo ina manufaa mengi zaidi kwa kuwa kama hakuna nyongeza kwa miaka mitano na sasa ikiongezeka maana yake itaongeza morali ya kazi.

Tunatarajia hata sekta binafsi italitazama suala hili kwa mtazamo chanja ili kuongeza morali ya kazi kwa wafanyakazi wake.

Matarajio ya wafanyakazi ni makubwa kwamba baada ya kilio cha muda mrefu, sasa faraja inakuja kwa kutangaziwa nyongeza ya mishahara au kuoungua kwa kodi ambayo nayo itatoa ahueni kubwa kwao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tanzania na kiu ya katiba mpya



Na Sabato Kasika

**MARA** baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita, wameibuka wanasiasa wanaopaza sauti wakimtaka Rais Samia Suluhu Hassan kujeresha mchakato wa katiba mpya.

Mchakato wa katiba hiyo uliishia njiani mara baada ya kumalizika kwa Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 ukiwa umefikia hatua ya kuandaa katiba inayopendekezwa.

Tangu wakati huo, kumekuwapo na juhudi mbalimbali zinazofanywa na wanasiasa za kutaka mchakato huo urejeshwe, ili nchi ipate katiba mpya, lakini bado hazijazaa matunda.

Kwa mfano, katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria yaliyofanyika jijini Dodoma, Mwenyekiti wa CUF Taifa, Prof. Ibrahim Lipumba, alimuomba aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli kukamilisha mchakato huo.

Alimweleza Magufuli kuwa, mambo makubwa aliyoyafanya na aliyokuwa akiendelea kuyatekeleza katika kipindi chake cha uongozi yataendelezwa na kulindwa endapo kutakuwa na 'katiba ya wananchi'.

Profesa Lipumba pia alipanga kumuombea kwa moyo wa dhati ili Mungu amupe nguvu katika kipindi hicho aweze kutekeleza viporo vyote alivyokuwa amebakisha, hata hivyo Magufuli amefariki lakini jukumu la kuandika katiba mpya bado halijafanyiwa kazi.

**Profesa Lipumba pia alipanga kumuombea kwa moyo wa dhati ili Mungu amupe nguvu katika kipindi hicho aweze kutekeleza viporo vyote alivyokuwa amebakisha, hata hivyo Magufuli amefariki lakini jukumu la kuandika katiba mpya bado halijafanyiwa kazi.**

Wakati akifikisha ombi hilo kwa Magufuli, chama chake kilikuwa kimetangaza kutoshiriki uchaguzi wa aina yoyote hadi ipatikane katiba mpya na tume huru ya uchaguzi.

Lakini pamoja nia hiyo wadau kutaka mchakato wa katiba mpya, pia walishawahi kuambiwa kuwa mchakato huo ni kiporo cha chakula kilichochacha hakiwezi kulika.

Ni Machi mwaka jana wakati akitembelea vyombo mbalimbali vya habari, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alikaririwa akisema hayo, baada ya kuulizwa na wana habari kupata maoni yake kuhusu mchakato huo.

Rais Samia, ameingia madarakani, maombi ya kurejeshwa kwa mchakato huo yameibuka kwa kishindo, huku wadau wakisema, wana imani naye, hivyo wanamuomba arejeshe upya mchakato huo.

Baadhi yao wameonyesha kuvutiwa na hotuba zake ambazo zimekuwa zikibeba ujumbe wa kuonyesha mwelekezo wa serikali yake, kuashiria mabadiliko anayotaka.

Huenda hotuba hizo zimekuwa kama kichocheo kwa wadau hao ambao wanapigia debe kurejeshwa kwa mchakato huo, ingawa mwenyewe ameshawaambia na kuwataka wasahau kwanza.

Kauli yake ya kuwataka wahasau kwanza, binafsi ninaichukulia kwa uzito mkubwa, kwani huenda anataka ajipe muda wa kutosha wa kukaa na kutafakari kuhusu mchakato huo na kisha aje na majibu kamili.

Kwa hali hiyo, si vibaya wadau hao wakatulia na kumpa nafasi kwanza ili akae na kutafakari ni nini cha kufanya au cha kuanza nacho kwenye utawala wake ambao bado haujamaliza hata mwezi.

Hivyo, wadau nao ni vyema wakatambua kuwa ndiyo kwanza rais anaendelea kupanga safu ya uongozi kabla ya kuendelea na mambo mengine ukiwamo huo mchakato wa katiba mpya.

Wakati mchakato huo Rais Samia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, Mwenyekiti akiwa Samuel Sitta.

Kwa hiyo ni imani ya wengi kuwa Rais anafahamu kikamilifu mwenendo mzima na hatua zilizopitiwa hadi kupata katiba iliyopendekezwa na pale mchakato ulipoishia na pengine anazo mbinu za mahali pa kuanzia ili kufanikisha kupata katiba hiyo.

# Spika: Ripoti TAKUKURU iwe inawasilishwa bungeni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameitaka serikali kuweka utaratibu wa kuiwasilisha Ripoti ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), inayotolewa kila mwaka.

Ripoti hiyo imekuwa ikiwasilishwa kwa Rais, huku wabunge wa wananchi kutopata nafasi ya kuipitia na kuhusishwa katika hatua za kukabiliana na tatizo la rushwa nchini.

Juzi jioni, wakati wa kuhitimisha mjadala wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka tano (202/22-2025/26) bungeni jijini Dodoma, Spika Ndugai aliwasilisha suala hilo kwa serikali akiitaka kulitazama.

"Hivi kwanini Ripoti ya PCCB (TAKUKURU) hailetwi bungeni? Kamati yetu ya PIC (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma) haina vitendea kazi vya kutosha," alisema.

Spika Ndugai pia aliitaka serikali kuona umuhimu wa kumtaka Msajili wa Hazina kuwasilisha bungeni taarifa ya taasisi anazozisimamia, huku akiutaka uongozi wa PIC kulishughulikia mara moja suala hilo.

Kimsingi, agizo hilo la Spika Ndugai ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya wiki iliyopita ya Taasisi ya WAJIBU iliyolishauri Bunge kuitaka serikali iwe inawasilisha bungeni ripoti hizo mbili (TAKUKURU na Msajili wa Hazina) ili kuimarisha uwajibikaji.

Alhamisi ya wiki iliyopita taasisi hiyo iliyo chini ya Mkurugenzi Mtendaji, Ludovick Utouh, aliyewahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuanzia mwaka 2006 hadi 2014, iliwasilisha kwa Spika Ndugai mapendekezo hayo mawili, ikilishauri yafanyiwe kazi ili kuongeza uwajibikaji nchini.

Yona Killagane, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya WAJIBU, aliwasilisha mapendekezo hayo kwa Spika Ndugai, wakati wa mafunzo kwa wajumbe wa kamati tatu za Bunge (PAC, LAAC na PIC) yaliyofanyika bungeni.

Alisema kwa kutambua PIC ni kamati changa, taasisi yao inapendekeza Bunge limtake Msajili wa Hazina awe anaandaa ripoti za taasisi zote anazizisimamia,kisha kuwasilishwa bungeni ili zifanyiwe kazi na kamati hiyo.

Katika pendekezo la pili, Killagane alisema kuna haja Ripoti ya TAKUKURU iwe inawasilishwa bungeni ili kutoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa.

"Taarifa ya PCCB (TAKUKURU) ni kazi nzuri na nyeti. Tunapendekeza iwafikie pia wananchi ili washiriki mapambano dhidi ya rushwa. Ripoti ya PCCB iliyowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 28 mwaka huu, iwasilishwe bungeni ili iwe wazi na ijadiliwe kuwapa fursa wananchi," Killagane aliwasilisha.

## Mrundikano wafungwa wachochea maambukizi TB

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, imebaini kuwa msongamano wa wafungwa na mahabusu unachochea kwa haraka maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) magerezani.

Kufuatia hali hiyo, Kamati imeshauri suala hilo lipatiwe ufumbuzi na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Akisoma maoni ya kamati hiyo, bungeni jana katika makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2021/22, Mwenyekiti wa Kamati, Fatuma Toufiq, alisema pia hatua za awali za upimaji na kuanzishiwa dawa kwa wanaokutwa na Kifua Kikuu zitumike ikiwa ni njia ya inayotumika katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema pia, umbali wa vituo vya kutolea dawa umechangia utoro wa kutumia dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

"Changamoto ya watu wanaoishi na VVU kutoroka matumizi ya dawa za kufubaza makali ya VVU kwa kiasi kikubwa umechangiwa na umbali wa vituo vya kutolea dawa, gharama za usafiri kutokana na watumiaji wengi kuwa wakazi wa maeneo ya pembezoni mwa halmashauri zao," alisema.

Kadhalika, kwa watumiaji wachache ambao ni wakazi walio karibu na maeneo ya upatikanaji wa dawa hizo, baadhi yao hutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu makazi yao na mawasiliano yao, kutokana na hali iliyopo ya unyanyapaa.

Katika hatua nyingine, Kamati ya Bunge ya Utawala Bora na Serikali za Mitaa, iliitaka serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC), ikamilishe haraka uandaaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uwekezaji ambao utatoa mwelekeo wa Taifa kuhusiana na masuala ya uwekezaji.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe (kulia) na Mkurugenzi wa Taasisi ya Al – Hekima, Shekhe Nurdin Kishik (kushoto), wakiwakabidhi bendera ya Taifa washiriki wa mashindano ya kimataifa ya kusoma Quraan, Abdallah Omary (wa pili kulia) na Omary Mohammed, wilayani humo mkoani Dar es Salaam jana, yatakayofanyika terehe 25, mwezi huu. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Serikali yachunguza sakata la waandishi kuwekwa chini ya ulinzi

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema imeanza uchunguzi wa tukio la Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam, Lusabilo Mwakabibi, anayedaiwa kuwaweka chini ya ulinzi wa polisi wanahabari.

Juzi, wanahabari wawili Christopher James wa Radio One pamoja na Dickson Billikwija wa Island Tv, wanadaiwa kuwekwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi kwa takribani saa tatu wakati wakitekeleza majukumu yao kwa agizo la Mkurugenzi huyo.

Akizungumzia tukio hilo, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema wizara yake inafuatilia malalamiko ya wadau wa tasnia ya habari dhidi ya Mkurugenzi huyo.

Waziri Bashungwa aliutaarifu umma na wadau mbalimbali wa tasnia ya habari kuwa wapole kwa kuwa wizara husika ipo katika hatua za awali za kufuatilia suala hilo.

"Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo tunafuatilia malalamiko ya wadau wa habari DED wa Manispaa ya Temeke, Mwakabibi, kuwaweka chini ya ulinzi wanahabari, tunaomba wanahabari wawe na subira wakati tuhuma hizi za kusikitisha zinafanyiwa kazi," alisema Bashungwa.

Sababu ya wanahabari hao kuwekwa chini ya ulinzi inaelezwa kuwa kulikuwa na kikao ambacho Mkurugenzi huyo alikiitisha na wafanyabiashara kutoka Soko la Mbagala Rangi Tatu, na wafanyabiashara hao waliamua kuwaita wanahabari hao ili wahudhurie.

Kutokana na wito huo, wanahabari hao walifika eneo la tukio kutekeleza majukumu yao kitendo ambacho kinadaiwa kilimkera mkurugenzi huyo na kudaiwa kuwaamuru askari kuwaweka chini ya ulinzi wanahabari hao hadi atakapomaliza kikao.

Taarifa za Mkurugenzi kuzuia waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao zimezua mjadala kwa wadau mbalimbali na kwenye vyombo vya habari, kwamba wengi wamekuwa wakihoji kuwa mkurugenzi huyo anatumia mamlaka yapi kuzuia waandishi kutekeleza majukumu yao, ikidaiwa kuwa siyo mara yake ya kwanza kukwazana na wanahabari.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WANUFAIKA WA MWISHO (BENEFICIAL OWNERS)**
**Dar es Salaam, Aprili 08, 2021**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) unapenda kuwataarifu Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara, kupitia Tangazo la Serikali Na. 189 la tarehe 12 Februari 2021 ameongeza muda wa miezi kumi na miwili (12) kuanzia tarehe 1 Januari, 2021 kwa ajili kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2020.

Takwa hili la kuwasilisha taarifa tajwa ni matokeo ya marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 yaliyofanyika kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 (Finance Act, 2020) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners).

Aidha Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, ambacho kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 kabla ya tarehe 1 Julai, 2020 kuwasilisha taarifa za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) ndani ya kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2020.

BRELA kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Kanuni za Wanufaika wa Mwisho (Beneficial Owners) zitakazoweka bayana utaratibu wa kukusanya na kuhifadhi taarifa hizi.

BRELA inawataka Wamiliki wa makampuni na umma kwa ujumla kutumia vizuri muda huu wa nyongeza kuwasilisha taarifa husika mapema na sio kusubiri muda wa mwisho ili kuepusha usumbufu wa namna yeyote unaoweza kujitokeza.

**Imetolewa na**
**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**

Jengo la Ushirka, Mtaa wa Lumumba, S.L.P. 9393, Dar Es Salaam, Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2212800, Nukushi: +255-22-2180371, barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz , Tovuti: www.brela.go.tz



Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa, akizungumza katika uzinduzi wa ofa ya Zantel wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, ambapo itawapatia wateja wake, uhuru wa kuwasiliana zaidi pamoja na maudhui ya Kiislam kama nukuu za Quran Tukufu na ujumbe wa kuwakumbusha wakati wa swala ili kuwawezesha waislamu kufanikisha funga zao. Kulia ni Meneja Masoko wa Zantel Zanzibar, Rukia Mtingwa. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# CWT yaweka msimamo kutoikubali bodi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimepinga uanzishwa wa Bodi ya Kitaaluma ya Walimu (Teachers Professional Board) na badala yake kimeshauri kubaki na Tume ya Utumishi ya Walimu (TSC) ili kupunguza utitiri wa vyombo vya kuwasimamia.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema sababu za kukataa kuanzishwa kwa bodi hiyo ni kutokana na uendeshwaji wake kutegemea pesa ya mwalimu mfukoni kwa ajili ya usajili, leseni na ada ya mwaka ambayo ni Sh. 50,000, gharama za kusikiliza mashauri ya semina kila mwaka ambayo ni lazima kuhuisha leseni.

"Ukishindwa kufanya hivyo mwalimu utalazimika kunyang'anywa leseni na kupoteza sifa ya kufundisha kwa sababu kanuni zilizotungwa sasa zinaelekeza hivyo," alisema Ulaya.

"Mbaya zaidi mtu akishindwa kufanya hivyo anafutiwa leseni yake, kitu ambacho kinaonyesha ni kunyanyasika kwa walimu na kumkandamiza kiuchumi," alisema.

Alisema sababu nyingine iliyowafanya kukataa Bodi hiyo na kutaka TSC iendelee ni kuimarishwa kwa kuwa inawasaidia kupunguza utitiri wa vyombo vinavyowasimamia walimu kwa ujumla.

"Hii bodi sisi walimu tunaendelea na msimamo wetu wa kuikataa, toka imeanzishwa msimamo wetu ulikuwa hivi hivi, lakini Bunge ilipitisha," alisema.

Alisema tayari wamewasilisha mapendekezo yao kwa kamati husika ya Bunge ambayo iliwaita viongozi hao kuwajulisha kuhusu upitishwaji wa bodi hiyo.

Hata hivyo, wamewataka walimu wote nchini kuwa watulivu wakati wakiendelea kusubiri majibu ya mapendekezo yao na msimamo walionao kuhusiana na uanzishwaji wa Bodi hiyo.

Alifafanua zaidi kuwa kulingana na unyeti wa sekta hiyo na kada hiyo ya ualimu serikali itazingatia maoni na mapendekezo yao ya hatua ya awali ya uundwaji wa sheria na kanuni zake.

Ulaya alisema mwaka 2019 CWT ilialikwa kutoa maoni kuhusu kuanzishwa kwa bodi hiyo, na ilikataa baada ya kuisoma sheria hiyo kwa kujiridhisha na kuona chombo hiko kililenga kumkandamiza mwalimu badala ya kusaidia.

"Tunaona kabisa majukumu yaliyopo kwenye bodi hiyo yanafafana na ya TSC, hivyo hatuna budi kuendelea na msimamo wetu wa awali wa kuikataa," alisema Ulaya.

Awali, akimkaribisha Rais wa CWT, Katibu wa chama hicho, Deus Seif, alisema suala la bodi linamgusa kila mwalimu na si walimu wanachama wa CWT.

Alisema chombo hicho kinasimamia masuala ya nidhamu, lakini mwalimu akitakiwa kukitumia inabidi atumie gharama zake mwenyewe jambo ambalo linamkandamiza kiuchumi.

"Kwanini tuwe na Bodi wakati tuna Tume ya Utumishi wa walimu, kwa hili sisi walimu haturudi nyuma," alisema Seif.

Naye Makamu wa Rais, Dinah Mathamani, alisema taaluma imeendelea kupanda juu na wao wanakiamini chombo cha TSC kiendelee kuwasimamia.

Naibu Katibu wa chama hicho, Maganga Japhet, alisema TSC, haijasema imeshindwa kutekeleza majukumu yake na CWT itaendelea kufanya kazi na tume badala ya bodi kama inavyoelekezwa.

# TANGAZO

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA | MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2020 | 31.12.2019 |
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,035 | 2,996 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,200 | 4,987 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 9,964 | 11,282 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,161 | 3,036 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 723 | 605 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 35,732 | 50,905 |
| 12 | Mali Nyingine | 9,808 | 5,180 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 434 | 556 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **67,055** | **79,546** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,489 | 18,274 |
| 18 | Amana za Wateja | 33,882 | 36,154 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 162 | 216 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 77 | 121 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,111 | 146 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 62 | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,197 | 4,558 |
| 28 | Madeni | - | |
| 29 | ***JUMLA YA DHIMA*** | **41,980** | **59,468** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **25,076** | **20,079** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,940 | 20,025 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 7,455 | 4,140 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (7,511) | (2,998) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,809) | (1,089) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **25,076** | **20,079** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,558 | 2,537 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 18,195 | 11,550 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,499 | 1,227 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 37% | 25% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 45% | 22% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 143% | 95% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 61% | 64% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 76% | 82% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -10% | -40% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.3% | -29% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 31.12.2020 | 31.12.2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 5,658 | 7,260 |
| 2 | Gharama za Riba | 2,615 | 3,384 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***3,042*** | ***3,876*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 1,808 | 400 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 2,468 | 584 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,299** | **1,329** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 128 | 70 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 178 | 542 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 993 | 718 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **5,261** | **5,653** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,122 | 2,019 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 136 | 267 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 3,003 | 3,368 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(5,195)** | **(1,432)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 1,386 | 343 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3,809)** | **(1,089)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(3,809)** | **(1,089)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 60 | 65 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (190) | (54) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (190) | (54) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 5 | 5 |
| | *BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI* | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -15.51% | -1.37% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -22.67% | -5.42% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 75.62% | 65.82% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 5.24% | 5.94% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | MWAKA WA SASA | MWAKA LINGANISHI |
|---|---|---|---|
| | | **31.12.2020** | **31.12.2019** |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (5,195) | (1,432) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 4,719 | 1,332 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 10,897 | 1,336 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (16,261) | (36,517) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (918) | 1,152 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3,439) | (3,973) |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - |
| | -SMR | 1,592 | 1,640 |
| | - Mengineyo | (21) | 219 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***(8,627)*** | ***(36,242)*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (13) | (83) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,817) | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(2,830)** | **(83)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 8,915 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **8,915** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(2,542)** | **(36,324)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 11,430 | 47,754 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **8,888** | **11,430** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **20,025** | - | **(4,086)** | **4,140** | - | - | **20,079** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (109) | - | | | (109) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (3,809) | | | | (3,809) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (3,315) | 3,315 | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 8,915 | | | | | | 8,915 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2020** | **28,940** | - | **(11,320)** | **7,455** | - | - | **25,076** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **20,025** | - | **(1,825)** | **2,445** | **396** | - | **21,041** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | 126 | | | | 126 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (1,089) | | | | (1,089) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (1,299) | 1,695 | (396) | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2019** | **20,025** | - | **(4,086)** | **4,140** | - | - | **20,079** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zilikaguliwa na BakerTilly "Certified Public Accountant" na kupata hati safi

| Jina | Cheo | Imesainiwa |
|---|---|---|
| Mr. Charles Rwechungura | Mkurugenzi | 31.03.2021 |
| Mr. Alfred Mkombo | Mkurugenzi | 31.03.2021 |

## NOTISI/ TANGAZO

**REAL MASTER COMPANY LTD,TAUSI AUCTION MART NA MASHOKA AUCTION MART** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki y**a AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| S/No | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DOMINA MARK MAHAMBO | OMARY NGUSA | NYUMBA | SHABAHA – MABOGINI KILIMANJARO | 30/04/2021 NAKUENDELEA |
| 2. | FATUMA RAMADHANI SENKONDO | FATUMA RAMADHANI SENKONDO | NYUMBA | MPIRANI-MABOGINI MOSHI-KILIMANJARO | 30/04/2021 NAKUENDELEA |
| 3. | ALEX SABAS SILAYO | ALEX SABAS SILAYO | NYUMBA | CHEKERENI-MABOGINI MOSHI-KILIMANJARO | 30/04/2021 NAKUENDELEA |
| 4 | WILIAM JACKSON KILEO | WILIAM JACKSON KILEO | NYUMBA | BOMANGOMBE KITONGOJI-NYERERE | 08/05/2021 NAKUENDELEA |
| 5 | AHMED ISSA KANDIRA | MIRIAM BALTAZARI TEMU | NYUMBA | BOMANGOMBE KITONGOJI-NYERERE | 08/05/2021 NAKUENDELEA |
| 6 | BRYSON SENYAEL SHOO | BRYSON SENYAEL SHOO | NYUMBA | BOMANGOMBE | 08/05/2021 NAKUENDELEA |
| 7 | HALIMA JUMA MZUNGU | MARIAM HARUNA MZUNGU | NYUMBA | BOMANGOMBE GEZAULOLE -HAI | 08/05/2021 NAKUENDELEA |
| 8 | NEEMA SOLOMONI MWANGA | NEEMA SOLOMONI MWANGA | NYUMBA | SINAI-KIA-SIHA | 15/05/2021 NAKUENDELEA |
| 9 | ALLEN BARAKAEL MMARI | ALLEN BARAKAEL MMARI | NYUMBA | FUKA-SIHA-SANYA JUU | 15/05/2021 NAKUENDELEA |
| 10 | SIMON ISMAEL MAWISH | SIMON ISMAEL MAWISH | NYUMBA | HIMO-NJIA PANDA MAGHARIBI | 21/05/2021 NAKUENDELEA |
| 11 | LIBERATY BERNARD SHAYO | LIBERATY BERNARD SHAYO | NYUMBA | HIMO -MOSHI | 21/05/2021 NAKUENDELEA |
| 12 | SELINA EZEKIEL MSHANA | SELINA EZEKIEL MSHANA | NYUMBA | UCHIRA -MOSHI | 21/05/2021 NAKUENDELEA |
| 13 | AWADHI JUMA AMIRI | AWADHI JUMA AMIRI | NYUMBA | KIFARU –MWANGA KILIMANJARO | 22/05/2021 NAKUENDELEA |
| 14 | ATHUMANI SADIKI MFINANGA | ATHUMANI SADIKI MFINANGA | NYUMBA | KIFARU –MWANGA KILIMANJARO | 22/05/2021 NAKUENDELEA |
| 15 | JUMA SELEMANI MNDEME | JUMA SELEMANI MNDEME | NYUMBA | KIFARU –MWANGA KILIMANJARO | 22/05/2021 NAKUENDELEA |
| 16 | REGINA WILLIAM MBOWE | REGINA WILLIAM MBOWE | NYUMBA | MACHAME | 29/05/2021 NAKUENDELEA |
| 17 | CHARLES PETER ULOMI | CHARLES PETER ULOMI | NYUMBA | MACHAME | 29/05/2021 NAKUENDELEA |
| 18 | ATILYO JOHN MWALONGO | ATILYO JOHN MWALONGO | NYUMBA | URU-KUSINI-KISOMBOKO | 05/06/2021 NAKUENDELEA |
| 19 | ANTHONI JOHN MUSHI | ANTHONI JOHN MUSHI | NYUMBA | URU-TAWINGO | 05/06/2021 NAKUENDELEA |
| 20 | JOROME VICTOR MUSHI | JOROME VICTOR MUSHI | NYUMBA | KIBOSHO MASHARIKI-MOSHI | 12/06/2021 NAKUENDELEA |
| 21 | SAMJI ATHUMANI KIMBWEREZA | SAMJI ATHUMANI KIMBWEREZA | NYUMBA | MAKANYA-SAME | 19/06/2021 NAKUENDELEA |
| 22 | CHACHA JOHNSON MATIKO | CHACHA JOHNSON MATIKO | NYUMBA NA ENEO | CHANIKA-NGOBEDI | 28/04/2021 NAKUENDELEA |
| 23 | NESTORY REVOCATUS NJAU | NESTORY REVOCATUS NJAU | NYUMBA | MVUTI-KIYOMBO | 29/04/2021 NA KUENDELEA |
| 24 | AMANI OMARY NOMBWANI | AMANI OMARY NOMBWANI | NYUMBA | KISARAWE II-KIGAMBONI | 30/04/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | EDON MGISHA ISAYA | EDON MGISHA ISAYA | NYUMBA | GEZA-KIGAMBONI | 30/04/2021 KUENDELEA |
| 26 | MINIHAJI H. MSHALE | MINIHAJI H. MSHALE | NYUMBA | ULONGONI 'B' | 04/05/2021 NA KUENDELEA |
| 27 | MAULID JUMANNE HAMIS | MAULID JUMANNE HAMIS | NYUMBA | IGOMA-MWANZA | 29/04/2021 NA KUENDELEA |
| 28 | EVOD FRANCIS MLINGA | EVOD FRANCIS MLINGA | T 444 DAY TOYOTA CROWN | MWANZA | 28/04/2021 NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754 443904 / 0752 868742 /0658 548684/0719351040/0689349477
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.


# TASAC kuanzisha mchakato kurekebisha tozo abiria bandarini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), inakusudia kuitisha vikao vya wadau ili kurekebisha kiwango cha tozo ya abiria wanaopita katika bandari ndogo zilizopo katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa bahari na maziwa.

Hivi sasa tozo inayotozwa ni Sh. 600, hivyo vikao hivyo vitakavyofanyika kabla ya mwisho wa mwezi wa sita mwaka huu, vitapunguza tozo hiyo.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Leonard Chamuriho, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Buchosa (CCM), Erick Shigongo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji, TASAC inatarajia kuitisha kikao cha wadau wa bandari za maziwa na bahari lini na utaratibu huu wa tozo mpya utaanza lini.

Dk.Chamuriho alisema vikao hivyo vitahusisha wadau wote wa bandari katika ngazi za kitaifa na kwenye maeneo husika wakiwamo wenye vyombo vya usafiri, abiria, mamlaka za Serikali za Mitaa.

"TASAC inakusudia kuwa tozo itakayoridhiwa na wadau itangazwe na kuanza kutumika mwaka mpya wa fedha wa 2020/21," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji, ni lini serikali itaacha kuwatoza Sh. 600 wakati wa kuingia na kutoka Bandarini wananchi wa visiwa vya Kasalazi, Yozu, Gembela na Soswa katika Jimbo la Buchosa kwa kisingizio cha uwekezaji.

Akijibu swali hilo, Waziri Chamuriho, alisema kiwango cha tozo ya abiria wanaopita katika bandari ndogo zilizopo katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa bahari na maziwa ni Sh. 600 kama ambavyo imeainishwa katika kitabu cha tozo cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA).

Alisema TPA baada ya kupokea malalamiko ya wadau mbalimbali kuhusu tozo hizo, imeanza kuchukua hatua za kufanya marejeo ya tozo hizo kwa bandari zote ndogo nchini kwa kushirikisha wadau katika maeneo mbalimbali.

# W'biashara kando ya barabara kuu kuendelea kuwezeshwa

BUNGE limeelezwa kuwa serikali itaendelea kutafuta namna bora ya kuwezesha wafanyabiashara waishio kwenye miji kando kando ya barabara kuu ikiwamo Mafinga kufanya biashara zao kwa saa 24.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alibainisha hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji, Serikali ipo tayari kuruhusu wananchi wanaoishi kwenye miji ambayo ipo kando ya barabara kuu kama Mji wa Mafinga kufanya biashara kwa saa ishirini na nne.

Naibu Waziri Silinde akijibu swali hilo, alisema serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali katika kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo ikiwa ni pamoja na kuwatengea maeneo kwa ajili ya kuendeshea biashara zao na kuwatambua kwa kuwapatia vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na watoa huduma.

Alitaja baadhi ya Halmashauri hizo ni Jiji la Dodoma, Jiji la Dar es Salaam na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Alibainisha kuwa uendeshaji wa biashara nyakati za usiku umeonekana kuwa na vikwazo vingi vya ulinzi na usalama wa wafanyabiashara, wateja pamoja na bidhaa zao.

Alisema uzoefu unaonesha kuwa maeneo zinakofanyika biashara kwa saa 24 kuna miundombinu yote muhimu ikiwamo taa, kamera, vyoo na maeneo ya kuhifadhia bidhaa za wafanyabiashara.

# STAMICO, TANESCO kuzalisha umeme MW 200

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), yameagizwa kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha mradi wa kuzalisha umeme zaidi ya MW 200 utakaotumia makaa ya mawe katika Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira.

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Jumbe.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani kuhakikisha wanautekeleza kwa wakati kutokana na mradi huo kuwa wa muda mrefu.

Akijibu swali hilo, Prof .Manya aliyaagiza mashirika hayo kutafuta fedha ili kukamilisha mradi huo na uanze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji, ni lini Serikali itaufufua Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira, pia ni lini baadhi ya waliokuwa Wafanyakazi wa mgodi wa makaa ya mawe Kiwira watalipwa stahiki zao baada ya mgodi huo kufungwa.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Manya alifafanua kuwa Mgodi huo ulikabidhiwa serikalini kupitia STAMICO mwaka 2013 kwa lengo la kuuendeleza.

"STAMICO kwa kushirikiana na TANESCO wanaendelea na mpango wa pamoja wa muda mrefu wa kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme zaidi ya MW 200 utakaotumia makaa ya mawe yatakayozalishwa katika Mgodi huo, makubaliano ya ushirikiano (MoU) kati ya STAMICO na TANESCO yako hatua za mwisho kukamilika kabla ya kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kisha kusainiwa,"alisema.

# Uwekezaji uwe makini ili kuepusha umaskini



Ukurasa 12



Ukurasa 14

Rais Joao Lourenco's wa Angola

siasa

JUMATANO APRILI 14, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

## MIAKA 37 BILA SOKOINE

# Alichosimamia kinabaki kuwa tunu kuu hadi leo

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI Mkuu Edward Sokoine, aliyefariki dunia Aprili 12, 1984 ametimiza miaka 37, tangu alipowaaga Watanzania, katika ajali ya gari iliyomaliza maisha yake, huko Dakawa mkoani Morogoro.

Ni takribani miongo minne, umri wa vijana wengi, ikiashiria kuwa vijana wengi hawamfahamu kiongozi huyo.

Taifa linapokumbuka mchango wake atakumbukwa kwa mengi ukiwamo msimamo wa kipekee katika historia ya viongozi wa Tanzania chini ya Mwalimu Julius Nyerere.

Alikuwa na mawazo, fikra, msimamo na mwelekeo mahsusi wa maendeleo ya nchi.

Alikuwa akisimamia masuala mbalimbali ya kijamii kama utamaduni, kilimo, uwekezaji na maendeleo vijijini.

Kwa mfano, katika hotuba zake mbalimbali, alisisitiza mambo muhimu kama uhuru wa kitaifa, kujitosheleza kwa chakula, kuwapo soko la kitaifa, uwekezaji katika kilimo na ufugaji na 'mapinduzi vijijini'

Linapokuja suala la uhuru wa kitaifa, msimamo wake ulikuwa wazi kuhusu umuhimu wa kulinda na kukuza uhuru wa Tanzania kama nchi na taifa na alitetea msimamo huo bila kuyumba.

### IMANI YAKE

Sokoine alimini kuwa, bila uhuru wa kitaifa, nchi haiwezi kuwa na maendeleo yanayoheshimu utu wa mtu kama binadamu, na alikemea wenye nia ya kuuza uhuru wa nchi zao ili waendelee kuishi lakini kuishi kitumwa.

Si hapo tu, bali pia katika utamaduni, mila na desturi, uzalendo, kujitegemea kama taifa, hakuamini kuwa mila na desturi zote ni nzuri ila alilaani zile za kuiga kutoka nje, hasa za Ulaya na Marekani, bila kujali uzuri au ubaya wake.



Waziri Mkuu Edward Sokoine, alipokuwa na mgeni wake kiongozi kutoka China. **PICHA: MTANDAO**

Katika hotuba aliyoitoa Oktoba, 1982, akiwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kule Arusha, alisema: "... jambo la tano ambalo ningependa nilitaje... ningewaomba wajumbe tusitupilie mila zetu nzuri mbali... utamaduni wetu na mila zetu umeingiliwa mno na mila na tabia za kigeni za kuwa na tamaa ya vitu, hasa visivyosaidia katika maisha".

Kwake, uzalendo ulikuwa ni moja ya sifa ya kiongozi bora, na kwamba ni muhimu kuchagua viongozi wazalendo ili walisaidie taifa kwa maana ya kuendeleza upendo.

Aliamini , uongozi siyo dhamana, bali pia kujitolea na kuwa mstari wa mbele katika vita vya kuwakomboa kimandeleo waliowengi, hasa walio vijijini.

### TAIFA KUJITEGEMEA

Taifa kujitegemea ilikuwa ni kama imani ndani ya fikra zake sera ya 'Ujamaa na Kujitegemea' ilikuwa msingi wa maendeleo ya serikali.

Ili kufanikisha sera hiyo, aliiondoa mara moja vikwazo wa kusafirisha chakula kutoka mkoa moja kwenda mwingine, kwa kuwa alipenda kujitegemea, akitumia maneno ya 'kusimama kwa miguu yetu wenyewe'.

Alikuwa kiongozi aliyechukia kuombaomba chakula kutoka nje, akiamini bila kujitegemea kwa chakula, nchi inakuwa tegemezi na kupoteza heshima, utu na uhuru mbele ya jamii za kimataifa.

Ili kujitegemea, alitamani kuwatumia wataalam na wasomi wa ndani badala ya 'kuwaabudu' wa nje na alitambua umuhimu wa kuwa na imani na wataalam hao na umuhimu wa utafiti wa kisomi kabla ya kufanya uamuzi wa kisera na kisiasa.

Yapo mengi ya kumuelezea kiongozi huyo, lakini muhimu kutambua kuwa alisisitiza kujitosheleza kwa chakula, soko la kitaifa na uwekezaji katika kilimo na ufugaji na aliamini kuwa chimbuko la maendeleo lilikuwa vijiji.

Hatua hiyo ndiyo iliyomfanya kuhimiza 'mapinduzi vijijini', kwa kuwa aliamini kuwa, vijiji vilikuwa ni chimbuko la kuleta mapinduzi ya kijamii, ya kiuchumi na ya kisiasa, na alitamani, baadala ya kuzalisha wataalam wengi zaidi, wakulima na wafugaji wageuzwe wawe ndio wataalam wenyewe.

### MFUATILIAJI

Kama ilivyokuwa kwa Rais John Magufuli kutoa maelekezo na kuyafuatilia, Sokoine pia alikuwa mfuatiliaji aliyefanya ziara za kushtukiza.

Kutoa maagizo na kuyafuatilia na ziara za kushtukiza, kuliwafanya watendaji wa serikali wanaotoa taarifa za uongo kutimiza wajibu .

Kwa wale ambao hawakuwapo kipindi hicho au walikuwa hawafuatilii utendaji wa kiongozi huyo, lakini wakawa wameshushudia utendaji wa Rais wa Awamu ya Tano, watakuwa wanajua kile ninachoelezea.

Wakati mwingine alikuwa akiwaita mawaziri ofisini kwake kumpelekea taarifa mbalimbali za utendaji na waliotoa taarifa za uongo, hakusita kuwaumbua na kuwachukulia hatua za kinidhamu.

Alichukia viongozi wazembe na wala rushwa, na aliwahi kutamka mwaka 1983 katika moja ya maelekezo yake kuwa; "Ole wake kiongozi mzembe nitakayemkuta. Viongozi wazembe na wabadhirifu wahesabu siku zao"

Si hapo ni bali sifa zake za ufuatiliaji wa ahadi au maagizo na kutoogopa mtu, zimejionyesha miaka ya hivi karibuni, hasa jinsi ambavyo watendaji wa serikali waliokwenda kinyume na uta

INAENDELEA UK. 12



Uwekezaji kwenye madini uzisaidie jamii jirani na migodi kupunguza umaskini. **PICHA: MTANDAO**..

# Uwekezaji uwe makini ili kuepusha umaskini

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibu serikali imesisitiza umuhimu mkubwa wa taifa kukaribisha na kukirimu wawekezaji kutokana na ukweli kuwa ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo taifa linaloyatamani hakuna mbadala wa uwekezaji .

Serikali inaamini kuwa ni kitu muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa taifa na kila nchi inahitaji wawekezaji wawe wa kutoka nje au wa ndani wenye mitaji ili kuanzisha na kuendeleza miradi mbalimbali ikiwamo viwanda, kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na uzalishaji wa aina zote kwa maendeleo.

Ni dhahiri hakuna anayepingana na nia njema ya kuwekeza lakini mazingira ya sasa yanahitaji umakini mkubwa katika mikataba ya kuanzisha miradi ya uwekezaji kwa vile Tanzania imeshaumwa na nyoka ni lazima kama ile methali inavyosema , aliyeng'atwa na nyoka akiona unyasi anashituka. Uwekezaji unaotazamiwa uwe na jicho pevu la kujua wapi taifa linapoumizwa au kunufaika.

Licha ya serikali kutaka wawekezaji na kuujua umuhimu wao , taifa linalazimika kujipanga na kuona lilipotoka kwenye kukaribisha wageni na kutoa fursa mbalimbali za kuweka mitaji yao kwenye vitega uchumi, likitumia darubini kali.

### USHAURI WA MKAPA

Serikali ya awamu ya tatu ilikuwa mstari wa mbele katika ubinafsishaji na kufungua milango kwa wawekezaji , na iliipoondoka madarakani iliacha ushauri . Katika kitabu cha Rais wa awamu hiyo Benjamin Mkapa cha "My Life, My Purpose" au kwa Kiswahili Maisha Yangu, Kusudio Langu, aligusia umuhimu wa kuanzishwa kwa baraza dogo ambalo ni sehemu ya bunge la kupitia miswada ya sheria na mikataba iliyopitishwa na chombo hicho kabla ya utekelezaji.

Pendekezo hilo ni muhimu kwa kuwa kila upande unataka kufaidika wawe wenye mitaji au wawekezaji na Watanzania wanaowapa rasilimali. Wakati serikali inapoamsha ari mpya ya uwekezaji ushauri huo ni muhimu. Kutumia wataalamu na kuangalia iwapo kuna tija. Hili ni kwa sababu wakati wawekezaji wanapokaribishwa kuna mahali wanaizidi serikali ujanja na kusababisha Watanzania kujiona kuwa hawanufaiki na kazi wanazozifanya, badala yake wanaambulia kuliwa badala ya kufaidi.

Ni wakati wa kutumia wataalamu na wabunge kuhakikisha kuwa uwekezaji haudhoofishi uchumi. Tena si wa kusaka manufaa ya kiuchumi kwa wachache hasa hao wanaotoa vibali vya uwekezaji na wawekezaji wenyewe kwani kama wafanyabiashara wanasaka na kulinda maslahi yao lazima kuwa makini, kama Mkapa alivyoshauri.

Ni wazi kuwa kunahitajika chombo makini cha wasomi, wachumi, wanasheria na wataalamu mbalimbali kutafsiri mikataba ya uwekezaji , mazingira na faida zitakazopatikana kwa vile imeonekana wawekezaji wakiachiwa kufanya watakalo huenda wasijali maslahi ya taifa na kuwashauri wabunge ili kufanya uamuzi.

### MUSTAKBALI WA TAIFA

Pamoja na kuwahitaji wawekezaji hao ni wakati wa kuwa na fikra za kuchochea maendeleo, kutafakari na kuibua hoja kuhusu mustakabali wa Tanzania itajikomboaje na kuachana na utegemezi? Taifa lina rasilimali za kila aina litazitumiaje kuendelea badala ya kuamini kuwa wanahitajika wageni kuziendeleza badala ya wazawa? Alishauri Mkapa.

"Unahitaji ukombozi wa pili, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni. Tunahitaji kama taifa na mtu mmoja mmoja kuona aibu kuwa na kuendelea kuwa ombaomba. Tunahitaji kujitegemea na kuthamini maendeleo endelevu " alisema Mkapa kwenye kitabu chake.

### KUTATUA CHANGAMOTO

Wakati mwingine inawezekana kuamini kuwa wawekezaji ni muhimu , lakini ukweli ni kwamba kuna hoja nyingi zinazohitajika kujibiwa kama unasaidia kupata ajira kwa vijana.

Ni swali la kwanza kwa vile mara nyingi zipo ahadi kuwa uwekezaji na vitega uchumi vinaongeza fursa za ajira, kulipa kodi na maendeleo, lakini muda mwingine sivyo.

Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ya mwaka 2019 inasema ukosefu wa ajira Afrika Kusini ya Sahara ni asilimia zaidi ya 6 ikimaanisha kuwa katika kila vijana 100, takribani 60 hawana kazi.

"Lakini hata kazi zilizopo ni za vibarua (unskilled) na za kiwango cha chini kwa sababu hakuna elimu wala ujuzi wa kufanyakazi kwa sababu ya ukosefu wa wasomi wenye viwango vya elimu ya juu, utaalamu unaohitajika na uchapajikazi mahiri wanaoutaka wawekezaji wageni.

Ukosefu wa miundombinu kama barabara, umeme, maji, reli, maghala ya kuihafadhi bidhaa, bandari, viwanja vya ndege, TEHAMA kunachangia ukuaji wa uchumi, kwa taifa moja moja, kanda na hata uwekezaji wa kigeni. Ni lazima kujiweka sawa kwenye miundombinu hiyo ili kuwa na msuli wa uwekezaji hasa wa mitaji ya kigeni.

Kwa mujibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) kadirio la dola bilioni 130 hadi bilioni 170 linahitajika kila mwaka kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu ya Afrika kila mwaka, jambo ambalo halijaweza kufanyika .

"Mkwamo huu ni riski kubwa kwa uwekezaji kwenye ukanda wa Afrika Kusini ya Sahara ..." inasema ADB hivyo kusisitiza kwanza umuhimu wa kuweka mazingira bora kwanza kabla ya kufikiria uwekezaji na mitaji ya kigeni.

# Alichosimamia kinabaki kuwa tunu kuu hadi leo

INATOKA UK. 11

ratibu walivyochukuliwa hatua za kinidhamu.

Mwaka 1983, Nyerere alizindua kampeni ya kupambana na wahujumu uchumi baada ya kupitishwa kwa Sheria ambayo iliendeshwa na kusimamiwa na Sokoine.

### AJALI HADI KIFO

Kiongozi huyo alifariki kwa ajali ya gari Aprili 12 mwaka 1984 wakati akitoka kwenye kikao cha bunge Dodoma kuelekea Dar es Salaam, eneo la Wami- Dakawa mkoani Morogoro.

Uongozi wake ulionekana kuwa wa mfano na kumfanya awe maarufu, kwa jinsi alivyokuwa na uadilifu na kufuatilia utendaji kazi, huku akikemea ulaji rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma.

Kifo chake kilileta majonzi makubwa kwa Watanzania wa kawaida ambao walikuwa wakimtarajia kama mtetezi wa wanyonge ambaye angeinua hali ya maisha yao, lakini 'akaondoka' mapema.

UCHAMBUZI

## ULAJI RIPOTI CAG

# Vigogo, wenye dhamana wanavyowatesa wanyonge

## ■ Ushuhuda; ulaji na 'makinikia' yake

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali (CAG) ya mwaka huu, inawatonesha wapigakura ambao wanazidi kuchoshwa na viongozi wenye dhamana ambao licha ya kuwagharamia kila kitu yakiwamo magari ya bei mbaya au mashangingi na V8, yenye viti vilivyofunikwa na vitambaa vyeupe yakiwabeba, wanaendelea kupora fedha za maendeleo badala ya kuboresha maisha yao.

Vigogo wanaokula kiyoyozi kwenye V8 ambao baadhi ni pamoja wakurugenzi mawaziri, manaibu na watendaji wakuu wa mawakala mbalimbali wanatajwa na CAG kuwa sio wawajibikaji bali wafujaji wa fedha za umma.

Miaka kadhaa iliyopita katika kampeni zake CCM, aliwahi kuahidi wananchi kuwa iwapo watachagua kuongoza nchi, itatoa Sh.milioni 50 kwa kila kijiji kwa ajili ya mikopo na kuwezesha wananchi kuanzisha miradi ya maendeleo.

Wengi walijiuliza serikali itazitoa wapi? Lakini, kabla hawajauliza wakati wanatafakari, walijibiwa kupitia majukwaa ya kampeni kuwa mgombea wake alikuwa ametumikia serikali kwa miongo mingi na alifahamu wapi fedha zilipo na alijua namna ya kuziingiza mikononi mwa wananchi.

Kiasi cha fedha kilichotajwa na CAG kuwa kimeliwa bila huruma na watendaji, mawaziri na viongozi wa serikali kwenye ripoti ya ukaguzi wa fedha za umma ya hivi karibuni ni kikubwa mno na pengine kingeweza kuvifikia vijiji vyote nchini kila kimoja kikivuna Sh. milioni 50.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu wa Serikali, inasema kuwa fedha zinachotwa na kutumiwa bila kufuata utaratibu na baadhi ya watuhumiwa ni Wizara ya Maliasili na Utalii , Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa , lakini pia Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa kuwaapisha wateule wakiwamo wakurugenzi wa mashirika ya umma, anawataja baadhi ya wajumbe wa bodi kuwa ni miongoni mwa wabadhirifu na walaji wa pesa umma.

Anaizungumzia bodi ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) akibainisha kuwa ni eneo moja ambalo fedha zimeliwa bila huruma pale wajumbe wa bodi walipofanya vikao zaidi ya 20 pia kujipa kazi kwa kujigeuza kuwa wajumbe wa kamati za utendaji na utekelezaji wa majukumu waliyojipangia ambayo yote yametumia mamilioni ya fedha lakini hakuna tija wala maslahi kwa taifa.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere. . **PICHA: MTANDAO**

Mchezo wa wizi wa fedha za umma umekuwa mwiba kwa maendeleo ya nchi kwa miaka mingi na licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa upotevu wa pesa za umma umekuwa saratani isiyopona.

Zipo hatua za kupunguza matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kama kupiga marufuku safari za ughaibuni ambazo wengi walizitumia kwa manufaa binafsi, kujilipa posho nyingi kila wakati zinazotokana na kuandaa semina na mikutano.

Ukweli ni kwamba wizi wa ubadhirifu wa fedha za umma ulionekana kwenye safari hizo maana wengi walipishana angani kuanzia watunga sheria bungeni, wafanyakazi wa serikali , wanasiasa, viongozi wa manispaa na halmashauri za miji na majiji wakiwamo mameya na madiwani.

Kwa ujumla waliosafiri walieleza kuwa wanafanya ziara za mafunzo kujifunza lakini kwa hakika huenda kwa miaka mingi walijikusanyia posho za kujikimu na hakukuwa na tija inayaoonekana kwa wizara zao, halmashauri zao, taifa wala kata wanazoziwakilisha.

> Zipo hatua za kupunguza matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija kama kupiga marufuku safari za ughaibuni ambazo wengi walizitumia kwa manufaa binafsi, kujilipa posho nyingi kila wakati zinazotokana na kuandaa semina na mikutano

Ripoti ya CAG ya sasa inaonyesha kuwa rasilimali za nchi kama serikali haitachukua hatua kali za udhibiti zitatumiwa kwa manufaa ya wachache kuneemesha wabadhirifu na wenye uzalendo wa kushibisha matumbo yao.

Ni wakati wa dola na vyombo vyake kuanzia sasa kusikiliza maelekezo ya CAG kudhibiti na kurudisha fedha zinazoliwa na wajanja kwa kuwa wanafahamu fedha za serikali zilipo na pia wanaelewa jinsi ya kuzipata na kuzirudisha mikononi mwa wananchi.

Kusikia madudu yaliyopo kwenye ripoti ya CAG haitoshi ni zama za kuiona serikali ikikata mirija ya kujichotea fedha kwenye wizara, serikali za mitaa na mashirika ya umma na mwanzo wa kuziba mianya mingine ya kula fedha za umma hasa kwa wale ambao wanageuza hazina ya serikali kuwa shamba la mwenda wazimu.

Viongozi wengine wanadaiwa kuwa wanalenga kujitafutia fedha ambazo huzipata hata kama hawakufanyakazi ndicho CAG anachobainisha kuwa wapo mawaziri wanaojilipa mamilioni kinyemela.

Suala hilo nalo liangaliwe kwenye utumishi wa umma ili kupunguza matumizi mabya ya fedha za umma yasiyo ya lazima tena yanayowanufaisha wachache wakati wapiga kura wanakosa huduma muhimu.

Kwa sababu Rais na Makamu wa Rais wamekuwa watumishi wa umma kwa muda mrefu, wanafahamu kuhusu mawaziri, wanasiasa na maofisa hao wanaojinufaisha wasinyamaziwe ili kudhibiti wizi wa pesa za umma.

Ripoti hii ya CAG ni eneo ambalo Watanzania wangetaka waone serikali ikilifanyia kazi ili kusafisha uozo na kuokoa mamilioni ya umma yanayopotea kila wakati kutokana na baadhi ya watendaji na viongozi kukosa uadilifu na uaminifu.

Ufisadi huo unapohusisha viongozi wengi kutoka ofisi mbalimbali unamaanisha kuwa mabilioni ya fedha yanaishia kwenye mikono ya wachache lakini maisha ya Watanzania wengi licha ya kutajwa kuwa yameboreka na imeingia kwenye uchumi wa kati yanaendelea kuzorota.

Iwapo viongozi watakuwa wanalipwa posho za kujikimu iwe wizarani, idarani au wakala kwa kazi ambazo hazikufanyika ni fedha kiasi gani zinapotea?

Ikiwa Tanzania imepitia kwenye miaka mitano ya udhibiti wa fedha za umma, kuanzia malipo kwa kontroli namba, kuhakiki mishahara ya watumishi wa umma dhidi ya wafanyakazi hewa, kukomesha safari za ughaibuni na kutumia njia za kisasa kukusanya fedha na mapato ya umma, inashangaza kuona kuwa ndivyo mchezo wa watumishi wa serikali kwenye sekta nyingi kujichotea pesa, tunajiuliza ni mamilioni mangapi yanaishia kwenye matumbo ya wachache?

Lakini pia kuna watumishi wengine wa serikali wana mchezo wa kuomba kamisheni au 'teni pasenti' kukwamisha wawekezaji kabla ya kuidhinisha iwe zabuni ama uanzishaji wa miradi, hao nao wanaendelea na mazoea hayo mpaka lini?

Kwa kufukuzia kamisheni wanasababisha kandarasi za umma kuwa duni, kusababisha manunuzi feki ya umma, huduma zisizoridhisha pamoja na kukosekana kwa thamani halisi ya fedha zinazotumiwa ikilinganishwa na bidhaa zilizonunuliwa au miradi ya kandarasi iliyofanyika.

Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango, anasema hatakuwa na huruma kwa wabadhirifu, wala rushwa na wanaoibia Watanzania maskini na kutokana na utumishi wake serikalini ni wazi hakuna aina ya wizi, ubadhirifu na dhuluma zinazofanyika serikalini asizozijua maana ameitumikia kwa muda mrefu ni tegemeo asaidie kuwafichua maana hakuna kipya watakachokitumia ambacho hakijulikani.

# Marais Afrika wanavyogeukana, kutosa watangulizi waliowaamini

Na Joseph Mwendapole

BARANI Afrika yapo mazoea ya viongozi wanaomaliza mihula yao kuwaachia madaraka jamaa wanaodhani watakuwa vibaraka wao wanapostaafu.

Katika mataifa mengi marais walioko madarakani wamewasimika wanaodhani ni vibaraka wa kulinda maslahi yao na familia zao ingawa wengi wamekuwa wakiwageuka.

Safari ya makala hii inaanza kuiangazia Angola, huko rais aliyetawala miaka 38, Jose Eduardo dos Santos alimpachika madaraka swahiba wake wa muda mrefu João Lourenço ili alinde maslahi yake.

Dos Santos baada ya kuiongoza Angola kwa miaka 38 kuanzia 1979 hadi mwaka wa 2017, alimkabidhi kijiti rafiki yake.

Mrithi wake alikuwa mtu wa ndani wa Dos Santos, mwanajeshi aliyehitimu nchini. Majenerali wote jeshini pamoja na rais mstaafu waliridhika kwa uteuzi huo.

Lakini ghafla na bila kutarajiwa Lourenço alipoingia ikulu alianza msako mkali dhidi ya watu mashuhuri na wenye ushawishi waliodaiwa kupora rasilimali za Angola.

Uzalendo huo uliwashtua waliokuwa washirika wa rais huyo mpya kwani alianza msako dhidi ya waliodaiwa kupora mali ya umma.

Hakumuogopa yeyote na mtangulizi wake na familia yake walijikuta katika wakati mgumu

Waangola wengi walijawa na matumaini kutokana na kasi yake lakini kwa wale waliooneka kulengwa na kampeni hiyo ya rais mpya hofu iliwajaa hata kulazimika kukimbilia nje ya nchi.

Lengo la kwanza na maarufu zaidi la kampeni hiyo lilikuwa kuisakama familia ya mtangulizi wake Dos Santos.

Iliwashangaza na kuwafurahisha Waangola wengi, ambao walikuwa wamechoka kutazama familia ya rais huyo wa zamani ikitajirika kutokana na mikataba ya serikali na kwa muda mrefu walikuwa wameogopa uongozi wa kifamilia ambao rais huyo wa zamani aliutengeneza kupitia mali na ushawishi wake.

Rais Lourenço - au JLo, kama anavyojulikana kwa Waangola alifanya kwa kasi na kwa fujo kudhibiti mali na mikataba iliyokuwa ikiinufaisha familia ya kwanza ya mtangulizi wake.

Isabel dos Santos binti wa mstaafu, aliondolewa kwenye kazi ya kuendesha kampuni kubwa ya mafuta ya serikali ya Sonangol.

Ndugu yake wa kambo alijikuta katika hatma kama hiyo kwa kuondolewa kama mkuu wa mfuko mkuu wa utajiri wa serikali na kuishi kizuizini na sasa anakabiliwa na kesi ya kujaribu kusafirisha nje Paundi milioni 500.



Rais Joao Lourenco's wa Angola, anayetikisa familia ya mtangulizi wake kwa ufisadi. **PICHA: MTANDAO.**

Kisha baadaye ukafuata msururu wa hatua kali zaidi dhidi ya familia ya Dos Santos ambapo mali za Isabela biashara zake zikaanza kuchukuliwa na serikali .

Kwa hatua hizo ambazo hakuna aliyezitabiri miaka ya hapo nyuma, familia ya Dos Santos ilisambaratishwa na mpango wake wa kuendelea kuwa na ushawishi katika uongozi wa Angola.

**MOTO DRC**

Mstaafu Joseph Kabila na Felix Tshisekedi, walianza kama marafiki Tshisekedi alichukua madaraka DRC Congo katika kile ambacho wengi walihofia kuwa ulikuwa mwendelezo wa utawala wa mtangulizi wake Joseph Kabila.

Chama cha Kabila kilifanya ushirikiano wa kisiasa na kile Tshisekedi, kumsaidia kushinda uchaguzi uliomfikisha madarakani .

Ilionekana kuwa haiwezekani kwa Tshisekedi kujitoa kutoka kivuli cha Kabila wakati aliposhika madaraka ya nchi Januari 2019, mwezi mmoja baada ya kushinda katika uchaguzi wa urais wakati kukiwa na shaka kutoka kwa waangalizi wa uchaguzi kwamba alikuwa amemshinda kwa kura nyingi mpinzani wa Kabila Martin Fayulu.

Tshisekedi alikuwa na nafasi ndogo ya kufanya ujanja lakini Kabila aliyekuwa madarakani tangu 2001 alikuwa ameimarisha udhibiti wa taasisi kuu za DR Congo.

Jeshi, huduma za ujasusi, mahakama ya kikatiba na Tume ya Uchaguzi, Chama cha Kabila cha Common Front for Congo (FCC) kilidhibiti theluthi mbili ya viti vya bunge na kumlazimisha Tshisekedi kuunda serikali ya muungano na chama chake cha walio wachache.

Lakini, miaka mitatu baadaye Tshisekedi alifaulu kuwafukuza kutoka nafasi kubwa na muhimu waliokuwa washirika wa mtangulizi wake Kabila na wabunge wengi wa FCC waljiunga na chama cha rais mpya ili kumpa uthabiti katika bunge

Wabunge hao walimtimua Waziri Mkuu aliyekuwa akiungwa mkono na Kabila Sylvestre Ilunkamba kwa kura ya kutokuwa na imani naye na kutoa ishara kwamba Tshisekedi, sasa alikuwa huru kutoka kwa ushawishi wa mtangulizi wake.

Kabila alikaa kimya katika mchakato wa kufutwa kazi kwa mshirika wake wa karibu Jeannine Mabunda aliyekuwa mkuu wa bunge, amekuwa akiishi katika shamba lake huko Katanga karibu na mpaka wa Zambia.

Kabila bado ni mashuhuri nchini DRC na yeye na familia yake wanadhibiti umiliki wa kampuni zaidi ya 80 zinazofanya kazi karibu katika kila sekta ya uchumi.

**BOTSWANA KWA KHAMA**

Katika hatua isiyokuwa ya kawaida nchini Botswana, rais wa zamani Ian Khama alipeleka vita kati yake na mrithi wake Mokgweetsi Masisi katika uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2019 Khama alikiunga mkono chama kipya kilichozinduliwa Mei 2019 cha Botswana Patriotic Front (BPF), ambacho kilipunguza wafuasi wa chama tawala cha Masisi.

Masisi alichukua hatua za kupunguza ushawishi wa mtangulizi wake kama rais wa zamani

Baba yake Khama, Seretse Khama alianzisha chama cha Botswana Democratic Party (BDP) mwanzoni mwa miaka ya 1960 na kimekuwa madarakani tangu 1966.

Ian Khama alighadhabishwa na Masisi, ambaye alimuunga mkono kuchukua nafasi yake kama kiongozi wa BDP, alichukua ushawishi wake kama rais wa zamani na kumtimua mshirika wake muhimu, mkuu wa zamani wa shirika la ujasusi, Isaac Kgosi, ambaye alifunguliwa mashtaka mbali mbali .

Uhasama huo wa kisiasa kati ya kiongozi wa zamani na mrithi wake uliitia Botswana katika hali ya wasi wasi hadi uchaguzi ulipofanywa na Rais Masisi akashinda muhula mwingine ndipo sasa mambo yalipotulia lakini kwa muda tu .

Khama anadaiwa kuendelea kuwaongoza pembeni viongozi wengine wa vyama vya upinzani wanaopinga utawala wa Masisi uhasama wao utazidi kudhihirika katika mapambano yajayo ya kisiasa nchini humo

BBC



## TBS yaendeleza ukaguzi maduka bidhaa chakula, vipodozi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MAOFISA wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Kanda ya Dodoma, wameendelea na ukaguzi wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi pamoja na kufanya usajili majengo hayo katika Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora, kwa lengo la kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa kufuata matakwa ya sheria pamoja na kuzingatia kanuni bora za afya ili kulinda afya za walaji.

Miongoni mwa majengo yaliyofanyiwa ukaguzi na usajili ni pamoja na migahawa, baa, mashine za kusaga, majengo ya kuuza vyakula na maduka ya vipodozi na zoezi hilo lilianza Machi 29, mwaka huu hadi Aprili 9, mwaka huu katika Wilaya za Sikonge.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi wilayani Sikonge, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS Dodoma, Zena Mushi, alisema katika ukaguzi na usajili wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi katika Wilaya ya Sikonge, wamefanikiwa kutoa vibali zaidi ya 100 kwa wafanyabiashara.

Alisema pamoja na changamoto za mtandao zilizopo maeneo ya vijijini, walifanikiwa kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa na kutoa vibali hivyo zaidi 100.

Alisema mwitikio wa wafanyabiashara kusajili majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi ni mkubwa hasa kutokana na elimu iliyotolewa kwa wananchi na wafanyabiashara kabla ya kuanza usajili tangu jukumu hilo likabidhiwe TBS kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

Alisema usajili wa majengo ya vyakula na vipodozi unafaida nyingi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha wafanyabiashara kutambulika kuwa wana vibali vya kusajiliwa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi.

"Lakini wengine kibali hicho kinawasaidia benki wanapokwenda kuomba mikopo, kwa sababu wakati mwingine wakitaka mkopo wanaambiwa leta kibali kinachokutambua kufanya hiyo biashara, kwa hiyo wakiwa nacho wanaweza kupata mkopo bila kikwazo," alisema Mushi na kuongeza;

"Kuna wafanyabiashara ambao wana tenda za vyakula kwa ajili kulisha taasisi mbalimbali kama vile shule, kwa hiyo wakati wa kuomba hiyo tenda, inabidi waambatanishe na kibali chetu, kwa hiyo inakuwa rahisi kwao kupata zabuni hiyo."

Alipoulizwa kama wananchi wa Sikonge walikuwa wakijua kama huduma ya usajili majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi inapatikana TBS badala ya iliyokuwa TFDA, Mushi alisema baadhi walikuwa wanajua hilo kwa sababu walikuwa wakiambiwa na maofisa biashara katika maeneo yao.

Kuhusu mkakati wa shirika hilo kufikia wafanyabiashara wote Kanda ya Kati, Mushi alisema mkakati wao ni kufikia wilaya zote za kanda hiyo, kwa sababu wana ratiba ambayo tayari imeandaliwa kwa ajili ya mwaka mzima.

# Mufti ataka mwezi Ramadhani kuombea dua viongozi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MUFTI wa Tanzania Shekhe Abubakari Zuberi, amewataka Watanzania kutumia kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kufanya dua kwa ajili ya kuwaombea viongozi wa serikali wapya walioingia madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake.

Mufti Zuberi, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati alipotembelea na kukagua ukarabati wa msikiti wa Gadafi.

Akizungumza na viongozi mbalimbali wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA), Mkoa wa Dodoma, baada ya kukagua ukarabati huo, alisema waumini wa dini hiyo wanatakiwa kutumia mwezi huo kufanya dua kwa ajili ya kuliombea taifa na viongozi wake.

"Katika kipindi cha Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ndiyo ambacho dua zinapokelezwa hivyo tuutumie kufanya dua kwa ajili ya taifa letu, lakini pia kuwaombea viongozi wetu wapya ili waliongoze taifa vizuri na kuleta maendeleo kwa Watanzania wote," alisema Mufti Zuberi.

Alisema muda huu ndiyo wakati mwafaka kwa Watanzania kuungana na kuwapa ushirikiano viongozi wa serikali waliopo madarakani.

"Tumuombee Rais wetu mama Samia Mungu ambariki amzungushie uzio wa kumlinda katika utendaji wake wa kila siku na ampatie ujasiri wa kutoa uamuzi yenye maslahi na taifa letu," alisema Mufti Zuberi.Pia, Mufti aliwataka viongozi wa dini ya Kiislamu nchini kujiunga na masomo ya Utawala pamoja na Teknolojia ya Habari na Mawasailiano (TEHAMA) ili kujiongezea ujuzi utakaowasaidia katika majukumu yao ya kila siku.

"Viongozi tunatakiwa kujiunga na kozi hii ambayo sisi Baraza tumeianda kwa ajili ya watu wetu ili kuwajengea uwezo katika mambo mbalimbali ikiwamo kuwa na uelewa namna ya kutambua itifaki mbalimbali," alisema Mufti.

Vilevile, alisema kuwa hivi sasa kutokana na viongozi wengi wa dini ya Kiislamu kutokuwa na elimu ya mambo ya utawala imekuwa ikiwapa wakati mgumu wanaposhiriki katika matukio mbalimbali ya kitaifa."Unakuta shekhe anakaa eneo ambalo yeye hastahili hali ambayo inatutia aibu sisi waislamu, lazima tupate mafunzo haya yatakayo tusaidia kutambua 'protocol' wapi ana kaa nani na wapi hakai nani," alisema Mufti.

Awali, Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema ukarabati wa msikiti huo unalenga kuboresha mazingira ili kuendana na hadhi ya Jiji la Dodoma.

"Hapa ndiyo yalipo makao makuu ya nchi hii hivyo wageni mbalimbali pamoja na viongozi wakuu wa nchi wapo hapa lazima tuwe na msikiti mkubwa na mzuri kwa ajili ya kufanya ibada," alisema Shekhe Rajabu.



Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zuberi (katikati), akizungumza na mashekhe wa Kata za Jiji la Dodoma juzi, wakati wa kikao cha kawaida cha utendaji kazi. Kulia ni Katibu wa Mufti, Mussa Hemed na Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ummy aliagiza jiji kuunda chombo uendeshaji miradi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameliagiza Jiji la Dodoma kuunda chombo maalumu kwa ajili ya uendeshaji wa miradi mikubwa ya kimkakati waliyonayo badala ya mfumo wa sasa miradi kuendeshwa na jiji ikiwamo kituo hicho kikuu cha mabasi.

Pia ametaka mfumo huo uwe rafiki kwa wateja, wajasiriamali pamoja na wafanyabiashara wa usafirishaji na badala ya kituo hicho kugeuka kero kwa wananchi wanapopata huduma.

Waziri Ummy alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara katika kituo kikuu cha mabasi Nanenane, na kusema lazima kiundwe chombo kwa ajili ya kuendesha miradi hiyo ili iweze kuleta tija kwa nchi kama malengo yalivyokusudiwa.

"Kuna mwongozo maalumu wa uendeshaji wa miradi hii, ili ilete tija, mimi nadhani kiundwe chombo maalumu cha kuendesha miradi hii ili tufikie lengo tulilokusudia, tunataka miradi hii izalishe mapato ili tukajenge shule, hospitali," alisema Waziri Ummy.

Alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 24 katika mradi huo wa stendi na kutaka usimamiwe kikamilifu ili itolewe huduma bora na mabasi yote yaanzie na kumalizia safari zake katika kituo hicho.

Alibainisha serikali itaendelea kujali wafanyabiashara wadogo na kama alivyoruhusu hayati Dk. John Magufuli kuwa wajasiriamali kufanya biashara katika kituo hicho ndivyo itakavyokuwa na kutaka wafanyebiashara zao kwa amani na kwa kufuata sheria.

Kwa upande wake, Meneja wa kituo hicho, Abedi Msangi, alisema kilianza kutoa huduma Juni 8, 2020 na kina uwezo wa kuhudumia mabasi 100 kwa wakati mmoja na mpaka sasa wameshakusanya Sh.milioni 680 katika shughuli zake.

Alisema walikusudia kukusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili mpaka sasa, lakini wamekusanya Sh. milioni 680 kutokana na mwitikio hafifu wa wafanyabiashara na wengine kuchukua vizimba na kutoanza shughuli katika kituo hicho.

"Kutokana na changamoto hii tumeamua kushusha kodi ya pango kutoka ya awali ya Sh. 15,000 kwa mita za mraba hadi kufikia Sh. 10,000 ili tuwavutie wateja kuanza kufanya biashara," alisema Msangi.

Naye, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema mpaka sasa mradi huo unasimamiwa na jiji, lakini wapo katika mchakato kuendesha kwa mfumo mwingine na wameshapeleka andiko ofisi ya mkoa ili kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa mradi huo na miradi mingine iliyopo katika jiji hilo.



# Mbeya yatekeleza mpango mkakati maendeleo kilimo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI Mkoani Mbeya, imeanza kutekeleza Mpango Mkakati miaka mitano katika sekta za kilimo (SZK), unaolenga kufanya mapinduzi kwenye sekta hiyo kwa kuongeza tija katika uzalishaji ili kuimarisha usalama wa chakula, kipato na lishe bora kwa wananchi.

Mpango huo unahimiza wananchi kuzalisha kwa kutumia njia za kisasa hasa kufanya kilimo cha kiushindani na cha kibiashara ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani pamoja na kukidhi mahitaji ya soko.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Maditto, aliyasema hayo jana alipokuwa anazungumzia mpango huo ulioanza kutekelezwa mwaka jana na utafikia ukomo mwaka 2025.

Alisema sababu ya kuanzisha mpango huo ni kutokana na maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo katika mkoa huo kutotumika ipasavyo yakiwamo yale ya umwagiliaji na tija ndogo kwenye uzalishaji.

Maditto alisema katika mkoa huo, maeneo yanayofaa kwa kilimo ni hekta milioni 1.7 lakini zinazotumika ni 577,054 ambazo ni sawa na asilimia 33.

Vilevile alisema katika mkoa huo, kuna hekta 108,332 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini eneo linalotumika kwa sasa ni hekta 54,606 ambazo ni sawa na asilimia 50.5 na kwamba baadhi ya maeneo hayatumiki kwa sababu ya teknolojia duni.

Alisema wastani wa uzalishaji wa mazao katika mkoa wa Mbeya ni tani milioni 3.18 lakini mahitaji ya chakula kulingana na idadi ya wananchi ni tani 549,531 sawa na asilimia 16.

"Kwa hiyo mkoa wetu kila mwaka unazalisha ziada ya chakula ya tani milioni 2.6, hivyo kwenye huu mpango wetu, tunahitaji kuongeza zaidi uzalishaji ili kuinua uchumi wa wananchi, mkoa na taifa na wadau mbalimbali wanashirikishwa," alisema Maditto.

Alisema kuna vyama vya ushirika 464 vinavyohusika katika sekta ya kilimo vikiwamo vyama vikuu, vyama vya msingi na vyama vya akiba na mikopo (SACCOS).Mpango huo, alisema unasisitiza matumizi ya teknolojia ambayo haiharibu mazingira na kwamba utekelezaji wa mpango huo unahitaji mabadiliko ya tabia na mitazamo ya wadau wakiwamo watunga sera.

Nao baadhi ya wadau wa sekta ya kilimo waliishauri serikali kuhakikisha inapowahamasisha wananchi kuzalisha mazao kwa wingi ihakikishe pia inawatafutia masoko ya uhakika ili wasipate hasara kwa mazao yao kukosa masoko.

Mmoja wa wadau hao, Linus Mlimba, alisema soko la mazao nchini hasa la chakula limekuwa si la uhakika hali ambayo imekuwa ikiwatia hasara wakulima kutokana na kuzalisha kwa gharama na kuuza kwa bei ambayo haiendani na gharama za uzalishaji.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita wakulima walikuwa hawanufaiki na kilimo kutokana na vizuizi mbalimbali vilivyokuwa vimeanzishwa na serikali ikiwamo kuzuia usafirishaji wa mazao nje ya nchi.

"Mpaka sasa kwenye mkoa wetu mahindi yanauzwa kati ya Sh. 6,000 na 8,000 kwa debe lakini soko lingekuwa vizuri kwa miezi kama hii, yangekuwa yanauzwa Sh. 10,000," alisema Mlimba.

Alisema wakati wa uzalishaji, serikali huwa haihusiki lakini baada ya mkulima kuvuna, ndipo serikali inaanza kuingia kwa kuweka vikwanzo mbalimbali.



Baadhi ya wawekezaji wenye asili ya China waliowekeza kwenye shughuli mbalimbali mkoani Mbeya, washiriki katika kikao maalumu kilichohusisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Kituo cha Uwekezaji (TIC) na wawekezaji hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TIC yatoa mwito kwa wawekezaji

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kimewataka wawekezaji wa ndani na nje wanaofanya shughuli zao kwenye mikoa ya ukanda huo kukitumia kituo hicho kutatua matatizo yanayowakabili badala ya kujifungia nayo.

Ofisa Uhamasishaji na Uwekezaji wa TIC Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ajerandro Sindano, aliyasema hayo juzi alipokuwa anazungumza na wandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu uwekezaji katika mikoa hiyo.

Alisema kituo hicho ni daraja kati ya wawekezaji na serikali, hivyo akawataka wawekezaji kuwasilisha kero zao mara kwa mara katika kituo hicho ili zitatuliwe mapema bila kuathiri shughuli zao za uzalishaji mali.

Sindano alisema yako maeneo mbalimbali katika ukanda wa Nyanda za Juu ambayo yanafaa kwa uwekezaji, hivyo akawataka wawekezaji wa ndani na nje kufika katika kituo hicho ili waelekezwe maeneo hayo na taratibu zinazotakiwa kufuatwa.

"Sisi ndio daraja ambalo linawaunganisha wawekezaji wetu na serikali kuu. Wawekezaji ambao wanakumbwa na matatizo wanatakiwa kupitia kwetu wanapotaka kuwasiliana na serikali. Kuna baadhi ya matatizo tunayatatua wenyewe bila kufika serikali kuu," alisema Sindano.

Sindano alisema kitabu maalumu kimeandaliwa kuelezea vivutio vya uwekezaji katika halmashauri zote za mkoa huo na kanda nzima kwa kuainisha kila eneo na vivutio vyake.

Alisema yako maeneo yanayofaa kwa wawekezaji kuwekeza kwenye kilimo, biashara, viwanda na shughuli zingine, hivyo akawataka wawekezaji wanaotaka kujitokeza ili wapewe taratibu.Hata hivyo, aliwataka wawekezaji wanaotoka nje ya nchi kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu za Tanzania wanapokuja kuwekeza kwa maelezo kuwa kila nchi ina taratibu zake tofauti na nchi zingine.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilikutana na wawekezaji kutoka China ikiwataka kufanya kazi kwa kufuata sheria huku ikiwahakikishia usalama wa mali zao.

# Kaya 8,950 zajiunga Mfuko bima ya afya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KAYA 8,949 zenye wanachama 37,528 zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii Iliyoboreshwa (iCHF) huku Halmashauri ya Jiji la Mbeya ikiongoza kuwa na idadi kubwa ya waliojiandikisha.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe juu ya mwitikio wa wananchi kujiunga na bima ya afya ya iCHF.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeandikisha wanachama 9,779 sawa na asilimia 2.5 kati ya Kata 2,288 zilizokuwa zimesajiliwa hapo awali.

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, alisema imesajili wanachama 7,839 sawa na asilimia 3.15, Chunya 5,095 sawa na asilimia 3.10, Busokelo 4,517 (asilimia 3.93), Mbarali 3,494 (asilimia 1.6), Wilaya ya Mbeya, wanachama waliosajiliwa 5,336 sawa na asilimia 1.76 na ya mwisho ni Kyela wanachama 1,468 sawa na asilimia 0.63.

Aliongeza kuwa kuanzia Desemba, 2019 hadi Novemba, mwaka jana, Sh. milioni 626 zilikusanywa kutokana na ada za usajili wa wanachama. Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 379 zililipwa kwa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, ununuzi wa vifaa, kamisheni kwa maofisa waandikishaji na ufuatiliaji shirikishi katika halmashauri.

"Malipo kwa vituo vya kutolea huduma za afya, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na rufani Sh. milioni 260 zilitolewa. Sh. milioni 24 zilipelekwa katika halmashauri kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa shughuli za CHF ngazi ya vijiji na mitaa, ununuzi wa vitendea kazi mfano kadi na vifungashio vyake, rejesta na vitabu vya madai ya matibabu na malipo ya kamisheni kwa maofisa waandikishaji ngazi ya vijiji na mitaa Sh. milioni 25," alisema Dk. Manyatta.

Alisema mkoa kwa kushirikiana na halmashauri na wadau, inaendelea kufanya uhamasishaji ili wananchi watambue umuhimu wa kujiunga na iCHF iliyoboreshwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alisema licha ya wilaya yake kutofanya vizuri katika uhamasishaji wa wananchi kujiunga na iCHF kwa mwaka 2019/20, wamejipanga kuongeza idadi ya wanachama.

Alisema hadi sasa wadau mbalimbali walijitokeza kuwalipia wananchi bima za afya wakiwamo Ibhasa Festival ambao waliwalipia wananchi 600.

# India yaikabidhi Z'bar msaada dawa za kansa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI ya India imeikabidhi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar msaada wa dawa za kutibu maradhi tofauti, ikiwamo kansa, zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 268.

Balozi mdogo wa India Zanzibar, Bhagwant Singh, alimkabidhi Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, shehena ya dawa hizo katika hafla iliyofanyika Bohari Kuu ya Dawa Maruhubi.

Balozi Bhagwant, alisema ushirikiano na uhusiano wa karibu kati ya India na Tanzania, ikiwamo Zanzibar, ulianza miaka mingi iliyopita na nchi hiyo imekuwa ikisaidia masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo elimu, afya, kilimo na ustawi wa wananchi.

Aliahidi kuwa India itaendelea kuimarisha ushirikiano kati yake na Tanzania kwa kutumia uwezo wa rasilimali walizonazo kusaidia kuimarisha uchumi wake.

Akipokea msaada huo, Waziri Mazrui aliishukuru Serikali ya India kwa msaada huo ambao alisema utapunguza kwa asilimia tatu ya bajeti ya kuagiza dawa nje.

Waziri Mazrui alimueleza Balozi mdogo wa India kuwa sehemu ya dawa hizo zitapelekwa kisiwani Pemba kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa kisiwa hicho.

Alisema Zanzibar kupatiwa msaada huo hasa dawa za kutibu maradhi ya kansa, ambazo zina gharama kubwa, utasaidia sana wananchi kupunguza safari za kufuata matibabu hospitali za maradhi hayo zilizopo Tanzania Bara na hospitali za nje ya nchi.

Alisema wizara yake imeandaa utaratibu mzuri wa kielektroniki unaohakikisha kuwa usambazaji wa dawa kutoka Bohari Kuu hadi kufika Hospitali na vituo vya afya unakuwa na ufanisi na hazipotei njiani.

Wakati huo huo, Waziri Mazrui amemuomba Balozi mdogo wa India kuwashawishi wawekezaji wa nchi yake kuja kuwekeza viwanda vya dawa Zanzibar ili kuondoa upungufu wa upatikanaji dawa nchini.

Aliahidi kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano unaohitajika kwa mwekezaji atakaeonyesha nia ya kuwekeza kiwanda cha dawa ili kuhakikisha lengo lake linafanikiwa.

Hata hivyo, alisema Zanzibar kuwa na kiwanda cha dawa ni jambo la msingi na alikumbusha kuwa miaka ya nyuma kilikuwapo lakini kutokana na changamoto zilizojitokeza kiwanda hicho kilisimamisha uzalishaji hadi hivi sasa.

# Hemed aonya askari washawishi migogoro ya ardhi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman ametoa onyo kali kwa baadhi ya askari wa vyombo vya dola wenye tabia ya kuwanyanyasa wananchi kwa sababu ya ushawishi wa migogoro ya ardhi.

Alitoa onyo hilo baada ya kusikiliza malalamiko ya pande zote mbili yanayohusisha mgogoro wa ardhi ambao kwa sasa uko mahakamani uliohusisha wakulima na msimamizi wa shamba liliopo Dole la Shadya Ahmed Abdulla.

Makamu wa Pili wa Rais alikuwa katika ziara ya kukagua shughuli za mandeleo na kufahamu changamoto zinazowasumbuwa wananchi ndani ya Wilaya ya Magharibi 'A' akimalizia ziara yake ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Akizinasihi pande zote mbili kuendelea kuwa na subira kipindi hichi ambacho tatizo lao liko mahakamani alikemea tabia ya baadhi ya viongozi na wananchi kutumia migogoro ya ardhi kuwanyanyasa wenzao na kutahadharisha kwamba askari yeyote atakayehusika na vitendo hivyo serikali itamuwajibisha na hata kumfukuza kazi mara moja.

Aliwataka wahusika wa mgogoro huo kusubiri uamuzi wa mahakama unaotarajiwa kutolewa ndani ya mwezi huu ili mwenye haki apatiwe fursa yake stahiki.

Akizungumzia sekta ya afya, aliwahakikishia wananchi wa Shehia ya Mbuzini, kwamba Serikali Kuu kupitia Wizara ya Afya na serikali ya mkoa na wilaya itajikita kuona huduma za afya ndani ya shehia hizo zinapatikana katika kipindi kifupi.

Alitoa mwezi mmoja na kuuagiza uongozi wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na uongozi wa ofisi ya mkoa Mjini Magharibi na Wilaya ya Magharibi kufanya utafiti utakaosaidia upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Shehia ya Mbuzini unatekelezwa ndani ya kipindi kifupi.

Alisema haipendezi kuona wananchi wanafikia hatua ya kuanzisha miradi ya ujenzi wa vituo vya afya kwa ajili ya kuondoa changamoto zinazowakabili hasa wajawazito, lakini hujitokeza baadhi ya watendaji wa taasisi za umma kuwa na tabia ya kukwamisha miradi hiyo kwa utashi wao binafsi.

Katika ziara hiyo ya Wilaya ya Magharibi 'A' Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alitembelea wakulima wa Bonde la Bumbwisudi, eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko Chuini Kwanyanya pamoja na wajasiriamali wanaojishughulisha na ukaushaji wa dagaa, Ngalawa.

Wakielezea changamoto zinazowakabili wakulima, wananchi na wajasiriamali hao walisema baadhi ya watendaji wa taasisi za umma wamekuwa kikwazo cha utatuzi wa changamoto zao zingine zikifika zaidi ya miaka mitatu.

Akifafanua baadhi ya changamoto hizo Makamo wa Pili wa Rais alitahadharisha kwamba mtendaji yeyote atakayebainika kuzorotesha maslahi ya wananchi kwa sasa anapaswa kutafuta kazi nyingine ya kufanya.

Alisema, akiwa Mtendaji Mkuu wa shughuli za serikali, ataendelea kufuatilia changamoto zote zinazowakwaza wananchi na mtendaji atakayebainika kusababisha uzembe wowote atalazimika kuwekwa pembeni.

Akitoa taarifa za Serikali Wilaya ya Magharibi 'A' ndani ya kipindi cha miezi mitatu, Suzan Peter Kunambi, alisema yapo maendeleo ya wastani yalioyopatikana katika sekta za kijamii na za kiuchumi.

HHHata hivyo, alisema zipo changamoto ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama, miundombinu ya Bara bara za ndani pamoja na umeme kwa baadhi maeneo ndani ya Wilaya hiyo.




Balozi Mdogo wa India Visiwani Zanzibar, Bhagwant Singh (kushoto), akimkabidhi Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazurui, moja ya boksi la dawa zilizotolewa msaada na nchi yake, katika hafla iliyofanyika Bohari Kuu ya dawa Maruhubi nje kidogo ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: MAELEZO-ZNZ**

# Jumuiya za wanawake zawaombea dua viongozi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JUMUIYA mbalimbali za wanawake visiwani hapa zimesoma dua ya kuiombea nchi pamoja na viongozi wakuu akiwamo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar.

Dua hiyo imesomwa katika ukumbi wa Idrisa Abdulwakili uliopo Kikwajuni na kuhudhuriwa na wananchi mbalimbali, viongozi wa serikali pamoja na wake wa viongozi akiwamo mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais na mke Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Baraza la Sanaa Zanzibar, Mariam Mohmed Hamdani, alisema dua hiyo imeandaliwa na wanawake kupitia jumuia mbalimbali lengo likiwa kuiombea Tanzania kuendelea kuwa na amani na utulivu pamoja na viongozi wakuu.

Alisema ni kawaida kwa binadamu kukutana kwa pamoja na kuombea kheri hususani katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani kumuomba "Allah" awaongoze katika mambo yaliyo mema na kuwajalia viongozi wa nchi akiwamo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar afya njema ili waweze kufanya majukumu yao kwa ufasaha.

Naye Naibu Spika wa Baraza la Wawawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, alisema wana imani na viongozi wakuu wa nchi wa serikali zote mbili kuwa watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa katiba zinazowaongoza ili kusukuma gurudumu la maendeleo kwa nchi zote mbili.

Alisema wana imani kubwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan atafanya mambo mazuri waliyokuwa wakiyahitaji wananchi.

Alisema Samia ni kiongozi mzoefu katika masuala ya siasa na wana matumaini kuwa pamoja na uzoefu wake utachangia kuleta chachu ya maendeleo katika nchi.

"Rais wa Jamhuri ya Munngano ni mwanamke wa kwanza kuwa rais kwa Afrika Mashariki, pia ni mtu mzoefu katika masuala ya siasa na hata mambo ya uongozi, hivyo hatuna wasiwasi ataliongoza jahazi na kuendeleza yale yalioachwa na hayati Magufuli," alisema.

Naye Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kadri siku zinavyokwenda jamii ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla inaendelea kujifunza kwa vitendo masuala ya uongozi kwa wanawake ikilinganishwa na hapo awali kwa kudhani haiwezekani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA INA VYUMBA VIWILI IPO KIJITONYAMA PLOT NAMBA 712/1 BLOCK 46 DAR ES SALAAM BEI 300M,MAZUNGUMZO YAPO.

## KIWANJA KINAUZWA - 1000SQM

Kipo Mbezi Luis 4 km toka Stand ya Mabasi ya Magufuli kina majengo 2, na kina hati (Offer ya miaka 99). Mawasiliano: 0712 600007 / 0777 655007. Bei maelewano.

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAURINE EDMUND WERIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1522/0027** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **SCOLASTICA** mwaka **2014**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/185614/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

VIOLET CHARLES MFUKO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili T 560 BBL,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa DSM/PHQ/R-B/182263/2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.88/2021**

Ombi la **ALLY ABDUL GANZEL** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MAHSEN SALUM GANZEL**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **19/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 06/04/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

JOSEPH ROBERT JACKSON ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA ISUZU WIZARD YENYE NAMBA ZA USAJILI T.857 BPG.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/183734/2021.

## KADI ZA GARI ZIMEPOTEA

EMMANUEL KATUBA MAYENGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA T 845 CAH. CHASSIS NO: FK629H532056. ENGINE NO: 6D171124871. KADI YA GARI NAMBA T 224 CUJ. CHASSIS NO SXA160035588. ENGINE NO: 3SO803558. YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: ARU/ARU/RB/185964/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SANLG WORLD WIDE INVESTMENT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 537 CHS** chasis namba **SLBSP JB535K 9005691** engine namba **SL157 FMI 19904441**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**KAH/TR/RB/501/2020**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.99/2021**

Ombi la **PETER C MHINA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **CECIL MNGANO MHINA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **20/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 13/04/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI WILAYA YA MOROGORO**
**MADAI NAMBARI 117/2021**
**Mdai: FRED SICHIZYA**
**ANAMDAI**
**MDAIWA: SALIMU WANJINGA**
**Kwa SALIMU WANJINGA**

Kwa kuwa Mdai/ Wadai * ameleta/ wameleta madai
*Yake/ Yao kwamba / Eleza hapa habari ya madai):
MADAI YA PESA 1,080,000/=
Kwa hiyo *nahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi
Katika Mahakama hii siku ya Jumanne tarehe
20 mwezi 4 Mwaka 2021 saa 2:00*asubuhi/ alasiri kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukataa shauri hilo ni lazima kuleta Mashahidi* wako/ wetu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea Katika shauri hilo.
Angalia kama*hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha
Kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa *wako/wetu na hati
Zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama *hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.
Mahakama ikithibitisha kama umepokea/ mmepokea kuitwa shaurini hii, in itaweza kutoa hukumu kuwa*umeshindwa/ mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 13/04/2020
FAHAMU
1.Iwapo *una/ mnafikiria kuwa mashahidi * wako/ wenu hawatahudhuria kwa hiari ya wenyewe
*Una/ mnaweza kupewa kuitwa shaurini katika Mahakama hii ya kuwalazima mashahidi wowote wahudhuria na kumpeleka hati yoyote ambayo inahitajiwa mbele ya Mahakama*una/ mnaweza kuomba Mahakama kwa kulipa Ada ipasayo
2.Iwapo* una /mna likubali deni hilo kuepukana na kutimilizwa kwa hukumu huenda ikawa juu*yao/ yenu au juu ya mali*yako/yenu au yote mawili
(a) Malipo yalipwe kwa Mdai / Wadai, au
(b) Malipo yalipwe katika Mahakama hii pamoja na Ada ya kazi hiyo.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu NATHAN MWESIGA Kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba T 244 DGP Engine namba 4GREAA3147. Chasis namba GRX1200013417. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU KWA KUMB.MWA/NY/R-B/172073/2021.

**Summons to appear (O.V.R. 20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO. 24 OF 2021**
**DR. JULIUS MASSAGA.........PLAINTIF**
**VICOBA GROUPS UNION TZ......DEFENDANT**
**TO: VIGUTA, NKURUMAH STREET**
**PLOT NO. 2035/155**
**CLOCK TOWER BUILDING 3RD FLOOR.**
**P.O. Box 95033, DAR ES SALAAM.**

WHEREWAS: The above named Applicant has/ instituted an Application against you, you are here summoned to appear in this Court in person or by Advocate or authorized agent on 28th day of April 2021 at 9:00 before Hon. B.S. MASOUD J. Chamber No. 07 in the morning to answer the said suit, and you are directed to product on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence. TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence. Give under my Hand and the seal of this court, the 9th day of APRIL, 2021.

**Summons to appear (O.V.R. 20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO. 24 OF 2021**
**DR. JULIUS MASSAGA.....................PLAINTIF**
**VICOBA GROUPS UNION TZ...................DEFENDANT**
**TO: CHRISTINA RWEBANGIRA**
**CAG HEAD QUARTERS**
**UKAGUZI STREET,**
**P.O. Box 450**
**DODOMA.**

WHEREWAS: The above named Applicant has/ instituted an Application against you, you are here summoned to appear in this Court in person or by Advocate or authorized agent on 28th day of April 2021 at 9:00 before Hon. B.S. MASOUD J. Chamber No. 07 in the morning to answer the said suit, and you are directed to product on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence. TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day the suit will be heard and determined in your absence. Give under my Hand and the seal of this court, the 9th day of APRIL, 2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARTY DOM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 454 DEZ Station- Wagon. Chassis namba 1C4PJMHS6EW23. Engine namba EW231238. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/MBA/RB/83527/2021.

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# 'Wanaombeza JPM washughulikiwe'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Mvumi mkoani Dodoma, Livingstone Lusinde (CCM), ameitaka serikali kuchukua hatua dhidi ya watu wote wanaombeza Hayati Rais John Magufuli.

Akichangia bungeni jana mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha, Lusinde alisema tabia hiyo ikifumbiwa macho kwa sasa, kuna hatari ikajitokeza tena kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mbunge huyo alisema kuwa kwa kiasi kikubwa mambo aliyofanya Magufuli yanaendelezwa kwa sasa na Rais Samia.

"Haiwezekani kuwavumilia watu hawa wanaomsema vibaya Magufuli maana hao hao watakuja kumsema vibaya Rais Samia, hii ni tabia, ujue kuna watu wanajua labda Samia alikuwa benchi akaingia kucheza mpira hapana, Rais Samia alikuwa anacheza na Magufuli, hivyo huwezi kuondoa legacy ya Magufuli Tanzania na Bara la Afrika haiwezekani," alisema.

Aliweka wazi kuwa wabunge wengi bila Magufuli wasingekuwapo ndani ya Bunge.

"Lakini jambo la kushanganza hata 40 haijafika tayari tumeshaanza kumsema vibaya, sasa hawa watu washike adabu na adabu iwashike na hatutaki warudie tena mambo ya kipuuzi," alisema Lusinde.

Aidha, Lusinde alihoji watu hao wanataka kaburi litikisike au kwakuwa miradi aliyoacha ina faida nyingi kwa nchi na inaendelezwa na Rais aliyepo madarakani kwa sasa.

"Tusiharibu image ya JPM kwa mambo ya ajabu wakati Samia anaendelea kutekeleza na



kukamilisha miradi iliyoachwa, tusimtangulie Rais maana ana maono yake kwa nchi," alisema.

Kuhusu mradi wa Bandari ya Bagamoyo, Mbunge huyo alisema Hayati Magufuli alieleza mabaya yaliyopo kwenye mkataba wake na kwamba watu waliobaki wanaweza kuyaondoa hayo mabaya yaliyopo.

Baada ya Lusinde kumaliza kuchangia, Spika Job Ndugai, alisema; "Kuna wabunge humu ndani darasa la saba wanasema wanaeleweka licha ya kuwa na elimu ya kawaida, hivi vitu vingine havina kazi, lakini kazi kubwa ya kufanya ni kwa wananchi na kibunge hivyo hizo elimu nyingine kubwa zitumike kufanyia tafiti, maprofesa muwe makini mnapozungumza," alisisitiza.

## Kanisa kujenga kituo chamafunzo kwa vijana

**Na Christina Mwakangale**

KANISA la Adventista wa Sabato Mzizima, linatarajia kuanza mradi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo kwa ajili ya vijana, kitakachogharimu Sh.bilioni nne.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kanisa, Jimbo la Mashariki Kati, Mchungaji Jonas Singo, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuwa kanisa hilo limekwishakusanya Sh. milioni 300 kwa ajili ya ujenzi huo.

Alisema kutokana na umuhimu wa kituo hicho, kanisa limeamua kushirikana na jamii kusaidia kukamilisha mradi huo na awamu ya kwanza, zinahitajika Sh. milioni 800 kwa ajili ya kununua eneo la ujenzi.

"Kituo hiki ni muhimu kitakuwa ni cha mafunzo ya wajibu na haki za raia, msaada wa kitaalamu juu ya kuushinda uraibu na vijana kuachana na dawa za kulevya na uhalifu.

"Kuna uhaba wa ajira ni tatizo hasa mijini, na hili limesababisha kuwapo matukio ya uhalifu, mimba zisizotarajiwa, magonjwa, tunahitaji kuwanusuru vijana," alisema Mch. Singo.

Pia, kitatoa mafunzo ya kuandaa chakula, lishe bora, kitengo cha mazoezi kwa jamii pamoja na kutoa ushauri kuhusu magonjwa ya kuambukiza na Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Kifua Kikuu (TB). Mwenyekiti wa Kamati ya Mradi, Josiah Mrimi alisema kituo hicho kitakapokamilika kitawachukua vijana wote watakaokidhi vigezo kujiunga na mafunzo kituoni hapo.

**Kuna uhaba wa ajira ni tatizo hasa mijini, hili limesababisha kuwapo matukio ya uhalifu, mimba zisizotarajiwa, magonjwa, tunahitaji kuwanusuru vijana.**




Mchungaji wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Mzizima, Charles Mjema (kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu harambee ya kuchangia ujenzi wa kituo cha Mvuto, kitakachotoa mafunzo mbalimbali kwa vijana ikiwamo ushauri dhidi ya utumiaji wa dawa za kulevya na uhalifu. Katikati ni Mkurugenzi wa Maendeleo wa kanisa hilo, Jimbo la Mashariki Kati mwa Tanzania, Mch. Jonas Singo na Mwenyekiti wa Mradi wa kituo hicho, Josia Mrimi. **PICHA: JOHN BADI**

## Mwanafunzi afia mtoni akichezea kandambili

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

MWANAFUNZI Aziza Dickson (7) anayesoma darasa la pili katika Shule ya Msingi Lubele, Kata ya Ikimba wilayani Kyela mkoani Mbeya, amefariki dunia baada ya kutumbukia katika mto Kiwila akiwa na wenzake wawili wakichezea kandambili.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Urlich Matei, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kwamba, kuna haja kwa wazazi na walezi kuwa waangalifu dhidi ya watoto wao katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha.

Alisema mtoto huyo amefariki huenda ni kutokana na uzembe wa wazazi ambao hawakuwa makini kuwakataza watoto hao kucheza kwenye maji, hivyo umakini unahitajika ili kulinda maisha ya watoto.

Akizungumza na Nipashe juu ya tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Lubele, Godfrey Mwambalile, alisema siku ya tukio alipigiwa simu na wasamalia wema majira ya saa kumi jioni kuwa kuna mtoto amezama mtoni.

Alisema baada ya kupokea taarifa hiyo alifika eneo la tukio na kujionea hali halisi, kuanza kumtafuta mtoto huo pasipo mafanikio.

Alisema wakati wanaendelea kumtafuta mtoto huyo, alitoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji Kata ambaye naye alifika eneo la tukio na kuanza kushirikiana naye kumtafuta mwanafunzi huyo, lakini jitihada za kumpata hazijazaa matunda.

Alisema chanzo mtoto huyo kufa maji ni baada ya watoto hao watatu walikuwa wakichezea kandamili na mmoja wao alizitupa eneo la Mto Kiwira uliokuwa umefurika maji.

Alisema mmoja wa watoto hao (Aziza) alienda kuzifuata bila kufahamu kuwa mto huo unakina kirefu, kujikuta akisombwa na maji.

Baba wa mtoto huyo, Dickson Minga alisema: "Nashangaa watoto walifikaje katika eneo hilo, ambao hawajawahi kufika hata siku moja".

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ikimba, Amani Mwailunga, alisema baada ya kusikia taarifa hizo alifika na kuungana na wananchi kuutafuta mwili huo pasipo mafanikio.

Alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwa makini kwa kuwatunza na kuwaelekeza watoto kutoenda kucheza kwenye maji.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kraudia Kitta, alipopigiwa simu ili kuzungumzia suala hili, simu yake ilipokelewa na mtoto wake akieleza kuwa mama hayupo.

# KANE KUONDOKA SPURS ISIPOFUZU UEFA




**LONDON,** England

STRAIKA wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, anatarajiwa kuiambia klabu hiyo anataka kuondoka ikiwa watashindwa kufuzu kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kwa mujibu wa Mirror.

Kane anazidi kuwa na wasiwasi juu ya Tottenham kushindwa kugombea mataji makubwa na hivyo anataka kwenda kutafuta changamoto mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hatatoa uamuzi wa mwisho juu ya maisha yake ya baadaye hadi baada ya mashindano ya Euro yanayofanyia msimu huu wa joto, ambapo atakuwa nahodha wa England.

Kane ana mkataba na Tottenham hadi Juni 2024 baada ya kusaini wa miaka sita mwaka 2018 wakati Mauricio Pochettino akiwa kocha.

Hata hivyo, mabosi wa Spurs mara zote wamenukuliwa wakisema kwamba, hawana mpango wala nia ya kumuuza mshambuliaji wao huyo.

Manchester United na Real Madrid zimekuwa zikihusishwa mara kwa mara na Kane, ambaye ni mfungaji bora wa nane katika historia ya Ligi Kuu England.

Huku pia bosi wake wake wa zamani hapo Spurs, Pochettino ambaye kwa sasa ni kocha wa Paris Saint-Germain, naye akionyesha nia ya kuwania saini yake.

# United wamtaka tena Sancho

**MANCHSTER,** England

KLABU ya Manchester United na kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer, bado hawajakata tamaa ya kumsajili winga wa England na Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

Mwaka jana, Man United walikuwa kwenye mstari wa mbele kuisaka saini ya winga huyo ila mwisho wa siku walishindwa kumpata nyota huyo mwenye umri wa miaka 21.

Ripoti zimeeleza kuwa mabosi wa 'Mashetani Wekundu' hao jicho lao la kwanza kwenye dirisha la usajili ni kwa Sancho na wanahitaji kumuona akiwa pale Old Trafford msimu ujao.

Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Dortmund, Hans Joachim wiki iliyopita aliweka wazi kuwa klabu hiyo inajiandaa kumuuza Sancho kwa ofa nzuri ambayo itafika mezani.

"Bado siwezi kujihusisha kwenye masuala ya kufikirika, hilo sio jambo zuri, lakini Jadon Sancho amekuwa bora muda wote ni sawa na Erling Haalad," alisema Joachim akinukuliwa na Bild.

"Nimezungumza na Jadon pia kuhusu suala hilo.

"Ikiwa kutakuwa na ofa nzuri lazima tujadili suala hilo pamoja na wakala wa mchezaji," aliongeza.

Kwa msimu huu licha ya kusumbuliwa na majeraha, Sancho ametoa jumla ya pasi 16 za mabao kwenye mashindano yote.




# Chelsea waongoza mbio kumsajili Aguero



**LONDON,** England

WAKATI mkataba wa nyota wa Manchester City, Sergio Aguero, ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ripoti za hapa London zinaitaja klabu ya Chelsea kuwa ndio inaongoza mbio za kumsajili.

Mwezi uliopita Man City waliweka wazi kuwa mchezaji wao huyo atakuwa anaondoka hapo kwenye dimba la Etihad baada ya msimu kuisha na amekuwa akihusishwa na klabu nyingi kubwa wakiwamo wapinzani wao kwenye Ligi Kuu England.

Licha ya kuwa na mapenzi makubwa na City, Aguero bado anatazamia kuwa anaweza kusalia England, baada ya klabu za Chelsea, Tottenham na Leeds United kutajwa kuwa mawindoni kuisata saini yake.

Kwa mujibu wa TyC Sports, Chelsea ndio wanaongoza kwa kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 raia wa Argentina.

Hata hivyo, Aguero ambaye amefunga jumla ya mabao 181 kwenye Ligi Kuu England, bado hayupo katika nafasi ya kufanya uamuzi juu ya hatma yake angalau hadi mwezi ujao.

Barcelona, Real Madrid, Paris Saint-Germain na Juventus zote zimetajwa kuwa zitaingia sokoni kuwasilisha ofa kwa nyota huyo wa zamani wa Atletico Madrid.

HABARI MICHEZO

# HAZARD KUWAKOSA TENA LIVERPOOL LEO




**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard leo Jumatano atakosa tena katika mchezo wa pili wa Real Madrid wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool, utakaopigwa pale katika dimba la Anfield.

Hazard amecheza mechi 14 msimu huu kutokana na kusumbuliwa na mejeraha na pia alikosa mchezo wa kwanza.

Raia huyo wa Ubelgiji alipona majeraha yake na kuingia akitokea benchi wakati Real Madrid ikishinda 2-1 dhidi ya Elche mwezi uliopita, lakini akaumia tena na kulazimika kuwa nje.

Hazard alirudi kwenye mazoezi mwishoni mwa wiki, lakini hakujumuishwa kwenye kikosi hicho cha 'Los Blancos' cha wachezaji 21 kwa ajili ya mchezo wa leo pale Anfield, ambapo timu hiyo ya kocha, Zinedine Zidane kwenye mchezo wa kwanza ilishinda 3-1.

Lucas Vazquez pia hatakuwapo kwenye mchezo huo kutokana na kuumia goti katika mchezo wa ushindi wa 2-1 wa Clasico dhidi ya Barcelona, Jumamosi.

Kulikuwa pia na hatihati kwa ufiti wa Toni Kroos kuweza kuwapo kwenye mchezo huo, baada ya kiungo huyo wa Ujerumani kutolewa nje kwenye mechi dhidi ya Barca, lakini alijumuishwa katika kikosi pamoja na Federico Valverde, ambaye pia ufiti wake ulikuwa na shaka.

## Dembele mambo bado Barca




**BARCELONA,** Hispania

WINGA wa Barcelona, Ousmane Dembele, amethibitisha kuwa hakuna taarifa yoyote ya ziada juu ya mazungumzo ya kukubaliana mkataba mpya na Barcelona.

Kocha Ronald Koeman amekuwa akisisitiza nia yake ya kutaka kumbakiza nyota huyo wa Ufaransa hapo Camp Nou wakati mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika msimu ujao.

Hata hivyo, hakujawa na maendeleo yoyote kwenye mazungumzo ya mkataba mpya, kwa mujibu wa Dembele kama alivyonukuliwa na gazeti la Marca.

Licha ya kuwapo na hali hiyo, Dembele mwenyewe bado ana matumaini kuwa hatma yake klabuni hapo itapewa umuhimu.

"Hakuna mazungumzo yoyote juu ya mkataba mpya, lakini najihisi vema tu," alisema Dembele akiliambia Marca.

Nyota huyu wa zamani wa Borussia Dortmund anafurahia msimu wake mzuri zaidi na Barcelona, akiwa sehemu ya ushambuliaji pamoja na Lionel Messi na Antoine Griezmann.

Dembele, 23, amebainisha kuwa kwa mwaka 2021 amefurahia zaidi kucheza kama mshambuliaji, na amecheza jumla ya mechi 24 za ligi kwa msimu huu wa 2020-21.




## *Neymar amshukuru Mbappe uzoefu Ligue 1*

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR amemshukuru mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe kwa kumsaidia kuzoea Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, akisema alimfundisha yeye 'kuwa Mfaransa'.

Nyota huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na PSG tangu mwaka 2017, akishinda mataji kadhaa yakiwamo matatu ya Ligue 1 na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Neymar ametengeneza upatina mzuri na Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ambaye amecheza naye tangu alipohamia hapo kutoka Monaco mwaka 2017.

"Alinifundisha kuhusu njia ya 'kuwa Mfaransa'... alinielezea namna ya kuwa Mfaransa," alisema Neymar akiiambia France Football. "Namshukuru sana kwa kunisaidia kuzoea maisha ya hapa, na hivyo furaha yangu ipo hapa."

Neymar amemsifia Mbappe kwa kumsaidia maisha binafsi na pia kwenye soka, na kumtaja kuwa kijana wa dhahabu wa PSG.

"Kwanza nilifurahi sana kukutana na huyu mtu hapa," alisema. "Kylian ni mtu mwenye utu sana, mara zote ana furaha na ana adabu kwa kila mtu.

"Ni kijana wa aina yake kwa hakika nafurahia sana kuwa naye hapa, maana najifunza vitu vingi kutoka kwake."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LINGARD AGOMBEWA KLABU KUBWA ULAYA

**West Ham kupigwa kikumbo na Madrid, PSG na Inter ambazo zimeonyesha nia ya...**

**LONDON,** England

MIAMBA ya soka ya Ulaya, klabu za Paris Saint-Germain, Real Madrid na Inter zimeingia kwenye mbio moja za kuwania saini ya Jesse Lingard, kwa mujibu wa ESPN.

**Lingard amekuwa kwenye kiwango bora na cha kuvutia tangu atue West Ham ambako anacheza kwa mkopo wa miezi sita aki tokea Manchester United.**

Na matokeo yake sasa, nyota huyo wa Kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 28, amezivutia klabu kubwa na sasa zinasaka saini yake ili kumsajili kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Lingard bado ana mkataba wa mwaka mmoja zaidi na klabu yake mama, Man United ambako alikuwa hana namba kwenye kikosi cha kwanza.

Lingard amefunga mabao nane katika mechi tisa na 'Wagonga Nyundo' hao wa London, ambao kwa mshangao hivi sasa wapo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

ESPN imeripoti kuwa, Lingard amekuwa akifuatiliwa kwa karibu na klabu hizo ili kumsajili, huku wao West Ham wakipambana kutaka kumpa mkataba wa kudumu.

Tayari Man United ilishawaambia West Ham kwamba, kama inataka kumsajili moja kwa moja Lingard inatakiwa kulipa pauni milioni 30.

West Ham inaweza kushindwa kutoa kiasi hicho cha fedha kutokana na ukweli kwamba, klabu nyingi Ulaya hali zake kifedha si nzuri kwa sasa kutoka na mlipuko wa virusi vya Corona uliozorotesha uchumi.

Na hiyo inaweza kutoa mwanya kwa PSG, Inter na Madrid kuwa na nafasi kubwa ya kuipata saini yake.

Lingard mwenyewe alinukuliwa wiki iliyopita na BT Sport kwamba, anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, jambo linalowezekana kumfanya kutimkia katika moja ya klabu hizo kubwa tatu Ulaya.

Hata hivyo, kama West Ham itamaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, itakuwa na nafasi pia ya kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

## ZISIKUPITE

### JUVE WAMTAKA DEMBELE

JUVENTUS wanampango wa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Ousmane Dembele, 23, mkataba wake utakapomalizika mwaka 2022. ***(Sky Sport Italia)***

### EDUARDO AWANIWA ARSENAL

ARSENAL bado wana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Klabu ya Celtic, Odsonne Edouard, 23, lakini wanakabiliana na ushindani kutoka Leicester. ***(Telegraph)***.

### UNITED WASITA KWA HAALAND

MANCHESTER United wanasita kuingia katika mazungumzo Borussia Dortmund juu ya usajili wa Erling Braut Haaland, 20, baada ya kushindwa kuafikiana bei nafuu kwa mchezaji mwingine wa timu hiyo, Jadon Sancho mwishoni mwa msimu uliopita. ***(The Athletic)***

### SPURS WAMTAKA BOATENG

TOTTENHAM Hotspur wanajiandaa kumsajili beki wa Bayern Munich, Jerome Boateng, 32. Mlinzi huyo wa kati ataondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Germany)***

### TOTTENHAM KUUZA NYOTA

KLABU ya Tottenham Hotspur itaelekeza nguvu zake katika kuimarisha safu yake ya ulinzi mwishoni mwa msimu, lakini itawapasa kwanza wawauze baadhi ya wachezaji wao ili kupata fedha za kusajili mabeki bora. ***(Mail)***

### TOMORI KUSAJILIWA JUMLA

AC Milan wana nia ya kumsajili moja kwa moja beki wa kati, Fikayo Tomori, 23, ambaye anaichezea klabu hiyo kwa mkopo akitokea Chelsea. ***(Corriere dello Sport, via Sport Witness)***

### LAMPARD ATAJWA PALACE

EDDIE Howe, Frank Lampard na kocha wa Burnley, Sean Dyche wapo kwenye orodha ya kupewa nafasi ya ukocha pale Crystal Palace kuchukua mikoba ya Roy Hodgson. Mkataba wa Hodgson unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

### MADRID YAACHIWA MILINKOVIC

KLABU ya Manchester United wamesitisha nia yao ya kumsajilili kiungo wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic, 26. Kiungo huyo pia anafuatiliwa na Real Madrid na PSG. ***(Gazzetta)***

### VAZQUEZ ANUKIA BAYERN

BAYERN Munich inawania kumsajili mlinzi wa Hispania, Lucas Vazquez, 29, ambaye anaweza asiichezee tena Real Madrid. Mchezaji huyo mwenye majeraha yake ya goti yanaweza kumweka nje hadi mwishoni mwa msimu huu, wakati mkataba wake utakapofikia mwisho. ***(Marca)***

### FERGUSON AMLIPUA OWEN

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson, amesema kiungo wa zamani, Owen Hargreaves ulikuwa ni usajili mbaya zaidi aliowahi kuufanya wakati akiwa klabuni hapo. ***(Star)***

# HABARI MICHEZO

## Namungo yageuzia msuli Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutofanya vizuri katika hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco amesema sasa hesabu zake anazihamishia kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kikosi cha Namungo ambacho mwishoni mwa wiki kilikubali kipigo cha pili mfululizo dhidi ya Nkana FC ya Zambia na cha nne mfululizo kwenye michuano hiyo, kimebakiza tu kukamilisha ratiba ya michuano hiyo kwa kucheza mechi mbili za mwisho dhidi ya Raja Cablanca ya Morocco hapa nyumbani na ugenini dhidi ya Pyramids ya Misri.

Katika mechi hiyo ya mwishoni mwa wiki Namungo ilikubali pigigo cha bao 1-0 baada ya mechi ya awali hapa nchini Nkana kuibuka na ushindi kama huo ikiwa ni baada wawakilishi hao wa Tanzania kupoteza dhidi ya Raja Casablanca na Pyramids, hivyo kuburuza mkia katika msimamo wa Kundi lao la D.

## JKU kazi inaendelea mazoezi Ramadhani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Ligi Kuu Zanzibar ikielekea mapumzikoni kupisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, timu ya JKU inayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, imesema haina mpango wa kufunga mpangilio wake mazoezi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Omar Khamis "Matu" amesema wametoa mapumziko ya siku kumi kwa wachezaji wa nje ya Zanzibar kwenda kuzitembelea familia zao na baada yao hapo wataendelea na mazoezi kama kawaida.

Alisema wamejipangia kufanya mazoezi mara moja kwa siku katika majira ya asubuhi katika uwanja wao wa Saateni huku wakiweka uwezekano wa kutumia viwanja vingine kutokana na hali ya hewa ya sasa kuwa ya mvua.

# WACHEZAJI YANGA WAZIDI KUBEBESHWA LAWAMA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI baadhi ya wanachama, mashabiki, wadau na wachezaji wa zamani wa Yanga wakionekana kuwanyooshea vidole vya shahada wachezaji wa Yanga kuwa hawajitumi na ndiyo maana hawapati matokeo mazuri, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro naye ameibuka na kusema, wachezaji wengi hawana vitu vya ziada kama ile ya zamani ambayo yeye alitumikia.

**Juzi beki wa zamani wa timu hiyo, Bakari Malima 'Jembe Ulaya', aliibuka na kuungana na baadhi ya mashabii wa timu hiyo wanaowatupia lawama mashabiki, akisema viongozi wanatekeleza wajibu wao kwa kuihudumia timu vizuri, lakini tatizo ni wachezaji kutojituma ipasavyo.**

Hata hivo, Muro ambaye alikuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa zamani kwenye klabu ya Yanga, amenukuliwa akisema hayo, akitoa tathmini fupi, baada ya Jumamosi timu hiyo kuambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC iliyowachefua wengi.

Alianza kuifananisha Yanga ya sasa na ile ya zamani ambayo yeye alikuwa msemaji akieleza kuwa ni vitu viwili tofauti.

"Ni kweli hatuendi vizuri na hii ni kutokana na jinsi timu ilivyo. Zamani tulikuwa tunaifananisha Yanga na timu kama Simba na klabu zingine bora, kubwa na maarufu Afrika, lakini si sasa kwa jinsi jina la Yanga lilivyo kubwa na hili linaloonekana uwanjani kwa sasa ni vitu viwili tofauti," alisema Muro.

Alisema jinsi jina la Yanga lilivyo na mpira wao inabidi uwe wa kimataifa na si timu ya kuanza kufungwa, halafu inatafuta bao la kusawazisha.

"Yanga si timu ya kuanza kufungwa halafu inaanza kutafuta bao la kusawazisha, kweli? Hii siyo Yanga. Yanga ni timu ya kushinda. Ni timu ya kampa kampa tena, kagongwa kagongwa tena na ikitokea sare, basi iwe mpira umeonekana, limepigwa shuti limegonga mtambaa panya, limepigwa limegongwa mwamba, au umembabua beki, hiyo ndiyo Yanga ya zamani na ndiyo tunayoitaka," alisema Ofisa Habari huyo maarufu za zamani.

Alionyesha kushangazwa na Yanga kuwa na baadhi ya washambuliaji ambao wana miezi mitano, wengine mwaka wakiwa hawajafunga bao.

"Kuna wengine hawajagongesha hata mwamba halafu unakaa unajiita mchezaji wa Yanga kweli? Mchezaji wa Yanga si awe mchezaji anayejua kudaka au kupiga mbele au chenga tu, inatakiwa iwe na wachezaji wenye vitu vya ziada. Huwezi kuifananisha Yanga na KMC. Yanga inatakiwa iwe na wachezaji ambao wana vitu vya ziada zaidi kuliko vile vya kawaida ambavyo wanavyo wachezaji wa timu nyingine," alisema.

Alisema haihitaji hata miwani kujua kuwa Yanga hii ina wachezaji wa kawaida sana, hivyo akataka umakini kwenye suala la usajili utakapoanza.

"Angalia wenzetu wale wa upande wa pili wamejiongeza, wana wachezaji ambao wana vitu vya ziada, ndiyo maana wamebadilika, huyu kocha wa sasa amekuja amekuta wachezaji wazuri, wenye uwezo na vitu vya ziada ya uwezo wa wachezaji wa kawaida, ndiyo umewafikisha hapa," alisema Mkuu huyu akiwazungumzia wapizani wao, Simba ambao wametinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.




Waogeleaji wa Klabu ya Taliss, wakishangilia na kuonyesha kombe la ushindi wa jumla baada ya kushinda mashindano ya Taifa ya Kuogelea yaliyofanyika kwenye bwawa la kuogelea la Klabu ya Gymkhana, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# *Taliss yakusanya medali 79 Kuogelea Taifa*

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya waogeleaji 21 wa Klabu ya Taliss wameiwezesha klabu hiyo kushinda jumla ya medali 79 katika Mashindano ya Taifa ya Kuogelea yaliyomalizika hivi karibuni kwenye bwawa la kuogelea la Klabu ya Gymkhana, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa na Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), medali hizo 79, kati ya hizo 35 ni za dhahabu, 21 za fedha na 23 za shaba.

Mashindano hayo yalishirikisha waogeleaji zaidi ya 90 na Taliss iliibuka na ushindi wa jumla kwa kupata pointi 1,826.

Meneja wa Taliss, Hadija Shebe alisema matokeo hayo mazuri yametokana na ufundishaji mzuri wa mkocha na mapokeo ya waogeleaji wakati wa ufundishwaji.

"Nawapongeza wazazi, walimu, makocha na wadau wote waliofanikisha timu yetu kushinda ushindi wa jumla kwa upande wa medali, haya ni mafanikio makubwa sana kwa timu na tusibweteke, tunatakiwa kufanya vizuri zaidi," alisema Hadija.

Matokeo hayo yanaonyesha, klabu ya Dar es Salaam Swimming Club (DSC) iliibuka ya pili kwa kupata jumla ya medali 48 ambapo kati ya hizo, 18 ni dhahabu, 18 nyingine ni fedha na 12 za shaba.

Nafasi ya tatu kwa upande wa kushinda medali nyingi imekwenda kwa klabu ya Mwanza iliyoshinda jumla ya medali 36 ambapo 16 ni za dhahabu, 14 (fedha) na sita za shaba.

Klabu ya nne ni Bluefins ambayo imeshinda jumla ya medali 57, kati ya hizo tisa ni za dhahabu, 23 za fedha na 25 za shaba.

Timu nyingine katika orodha hiyo ni FK Blue Marlins iliopata medali 20, ikiwa tisa ni za dhahabu, tano za fedha na sita za shaba wakati timu ya Mis Piranhas ilishika nafasi ya sita kwa kupata jumla ya medali 14, tatu zikiwa za dhahabu, nne za fedha na saba za shaba.

Michezo
Jumatano Aprili 14, 2021
Nipashe



Lingard agombewa klabu kubwa Ulaya UKURASA 22

KAZINI LEO...



Wachezaji wa Simba, mshambuliaji, Chris Mugalu (Kushoto) na kiungo, Taddeo Lwanga, wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Simba Mo Arena, Bunju - Dar es Salaam. Timu hiyo itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuikaribisha Mtibwa Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara.
**PICHA: SIMBA**

## Mwambusi agawa dozi gonjwa Yanga

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema amefanyia kazi kasoro zilizojitokeza katika mechi iliyopita na sasa akili na nguvu zao wanazielekeza katika kusaka pointi tatu kwenye mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema amefanyia kazi kasoro hizo hasa safu ya kiungo na ulinzi ili kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi.

Alisema iko wazi kwamba wanaongoza ligi na wachezaji wana morali wa juu, hivyo sasa wanasahau matokeo yaliyopita na wanaenda kusaka pointi tatu muhimu katika mechi ijayo.

"Baada ya kupata sare dhidi ya KMC FC, tumeenda kufanyia kazi upungufu wetu ikiwamo maelewano ya safu ya kiungo, namba sita, saba, nane pamoja na safu ya ulinzi ambayo katika mechi iliyopita tulifanya mabadiliko madogo.

"Sasa tuko sawa na tayari kwa ajili ya kwenda kutafuta pointi muhimu na ushindi katika mchezo huo ili kujiimarisha katika kilele tuliyopo na kuendelea na mipango yetu ya ubingwa," alisema Mwambusi.

# GOMES ATANGAZA MECHI NNE ZA KUISHUSHA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

●●● Kuanza na Mtibwa leo kwa Mkapa, awachambua pia Waarabu wa Algeria na Kaizer Chiefs CAF, asema...

WAKATI leo wakirejea Ligi Kuu Bara kwa mara ya kwanza baada ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema ana uhakika watazitumia vema mechi nne zilizopo mbele yao kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo kwa kuwa malengo yao makubwa ni kutetea ubingwa huo.

**Simba ambayo itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa 1:00 usiku kuikaribisha Mtibwa Sugar, imefuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa kileleni mwa msimamo wa Kundi A, lililokuwa likimjumuisha bingwa mtetezi, Al Ahly ya Misri iliyomaliza na fasi ya pili, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan iliyoburuza mkia.**

Baada ya mechi ya leo, Simba itashuka katika Uwanja wa Kambarage mkoani Shinyanga Jumapili kuivaa Mwadui FC, kisha siku tatu baadaye itapambana na Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoka kabla ya Aprili 24, mwaka huu kutua jijini Mwanza kuvaana na Gwambina FC.

Hadi sasa Simba ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 46 baada ya mechi 20, huku Yanga ikiwa kileleni na alama zake 51 zilizotokana na michezo 24 wakati Azam FC iliyoshuka dimbani mara 25, ikiwa na pointi 47 katika nafasi ya pili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, katika mahojiano maalum na mwandishi wetu juzi, Gomes alisema baada ya mechi nne zijazo kuanzia ya leo dhidi ya Mtibwa Sugar watakuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

"Yaliyopita yamepita tumefuzu robo fainali ambayo tutacheza mwezi ujao, kwa hiyo tuna muda wa kujiandaa, sasa tunataka kuelekeza nguvu kwenye ligi kwa sababu ligi ni lengo letu kuu, lazima tuchukue nafasi ya kwanza haraka, tunataka kucheza Ligi ya Mabingwa kila mwaka.

"Natarajia utashi na hamasa kubwa kwa wachezaji wangu na ninahakika nitacheza na wachezaji wangu bora," alisema kocha huyo raia wa Ufaransa.

Kuhusu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Gomes alisema: "Kwa ukweli tuna furaha kufika robo fainali kwani kundi letu lilikuwa gumu sana, tulianza kwa kucheza mechi ngumu na kiufundi mkubwa dhidi ya AS Vita, na kisha tukampiga Al Ahly hapa nyumbani, ninauhakika kwa sasa Simba ni moja kati timu bora Afrika, hivyo kwa sasa hatumhofii yeyote.

"Tunaziheshimu timu zote, tupo huru kucheza na timu yoyote, CR Belouizdad na MC Alger nazijua vizuri maana nilifundisha soka Algeria pia Kaizer Chiefs naifahamu, hatutakiwi kuchagua, Mungu atatupa timu moja baada ya hapo tutatakiwa kucheza kwa kujiamini na heshima. Katika mashindano ya CAF tunaweza kuvuka robo fainali kama tutakuwa na nidhamu na kucheza kwa nidhamu kama ambavyo tunacheza wakati wote," Gomes alisema.

Kocha huyo alisema hajutii kuondoka Al-Merrikh Januari na kujiunga na Simba na amekuwa akishangazwa na hamasa kubwa kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo hususan katika mechi dhidi ya Al Ahly wakishinda bao 1-0.

"Ni ajabu, uwanja ulijaa mashabiki na kiukweli walitupa nguvu, kama unataka kwenda mbali kwenye mashindano ya Afrika na Ligi ya Mabingwa, unahitaji mashabiki wenye hamasa, tuna kazi ya kufanya na Simba, na nina hakika tukiwa pamoja katika televisheni na uwanjani, tunaweza kutengeneza njia nzuri katika mashindano haya.

Lakini kuelekea mechi ya kesho, kwa upande wa Kocha wa Mtibwa Sugar, Vincent Barnabas, yeye alisema Simba ni miongoni mwa timu bora Afrika kwa sasa ambayo inacheza vizuri kwa pamoja, lakini wamejipanga kuona ni namna gani watawakabili.

"Utakuwa ni mchezo mzuri wa kufunguka zaidi kwa sababu timu zote zinacheza, kama unajua Mtibwa ni timu ya kucheza na Simba na wenyewe ni timu ya kucheza," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >